# ANUWAI YA KIBIBLIA:

*Mtazamo wa Mungu kuhusu Majukumu ya Wanaume na Wanawake*

(**Biblical Diversity:** God's View of the Roles of Men & Women**)**

**Louis & Bonnie Rushmore**

©2016 Louis Rushmore

©2024 (Swahili)

Kimechapwa na / Printed by:
World Evangelism Media & Missions
705 Devine Street
Winona, Mississippi 38967

Nakala ya Kiswahili / Swahili Copy
Swahili Gospel Team
+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 765 098 981

www.gospelgazette.com
www.WorldEvangelismMedia.com

HAKIUZWI / NOT FOR SALE

# Dibaji

Kwa miaka mingi kumesemwa mengi kuhusu *umoja katika utofauti*. Hata hivyo, mara kwa mara, makosa ya kibiblia yamekuwa yakifundishwa katika jaribio la kubadili *muungano* na makanisa yaliundwa na wanadamu kuwa *umoja* wa kimaandiko. Daima nimependa kielelezo kimoja cha jinsi paka wawili jinsi walivyofungwa mikia yao pamoja na kutupwa juu ya kamba, wanaweza kuwakilisha muungano, lakini hali kama hiyo haitaonesha *umoja* kamwe. Kuita *umoja* kile ambacho ni matakwa ya mtu hakutaleta *umoja*. Vivyo hivyo, kuita jinsi mtu awezavyo, muungano wa watu wa Mungu na watu wasioona Biblia pekee kuwa ndiyo yenye mamlaka (2 Timotheo 3:16-17; 2 Petro 1:3), ambao hawakubaliani na mwongozo wa Yesu kuhusu wokovu, (Marko 16:16), ambao hawaabudu "katika roho na kweli" (Yohana 4:24), wasiojipanga wenyewe kuwa makusanyiko yanayojitegemea (Matendo 14:23) na kadhalika wala sio wawakilishi wa *umoja* wa kweli wa kiroho wala hawana utofauti wa kibiblia.

Hata hivyo, majukumu husika ambayo Mungu amewagawia wanaume na wanawake katika kanisa na nyumbani yanawakilisha picha halisi ya utofauti wa Biblia. Kwa hali hiyo, yaliyomo katika kitabu hiki yanawasilishwa kwa unyenyekevu na heshima ili msomaji apitie na kujifunza kwa matumaini kwamba wanaume na wanawake Wakristo watajengwa kutokana na kitabu hiki. kwa kuyakumbatia kikamilifu, majukumu ya wanaume na wanake yatachangia zaidi katika makanisa yenye nguvu na nyumba zenye furaha.

Sehemu ya pili ya kitabu hiki, iliandikwa na marehemu mke wangu, iligunduliwa mwaka mmoja baada ya kifo chake Bonnie Sue Rushmore (1956 – 2015). Sikumbuki kuona makala hiyo hapo awali, ingawa najua kwamba aliwahi kufundisha kuhusu somo hilo katika

semina ya hamasa ya wanawake na nje ya nchi katika safari za umisheni. Anaendelea kutoa mchango wa thamani na wenye kujenga iwe karibu au mbali (Waebrania 11:4).

Bila ya kudharau njia nyingine za mawasiliano ya watu wengi, ukurasa uliochapishwa upo tayari pindi mpokeaji atakapokuwa tayari kuupokea. Vitabu huenda mbali zaidi na hudumu kwa mudamrefu zaidi kuliko sisi wanadamu tuwezavyo kufanikisha wenyewe. Bonnie ameacha nyuma ushawishi wa kiroho na njia ambazo kwa hizo hata sasa anashiriki katika kuwajenga wengine. Natumaini kufanya vivyo hivyo siku moja.

**Louis Rushmore, Mwinjilisti**

# YALIYOMO


**Wajibu wa Wanaume:**............................................................ 6

Uongzi wa Kiume katika Kanisa ........................................................ 7

Uongozi wa Kiume katika Uaskofu .................................................. 14

Uongozi wa Kiume katika Nyumba .................................................. 53

**Wajibu wa Wanawake:**.......................................................... 66

Wajibu wa Wanawake katika Kanisa ................................................ 67

Wajibu wa Wake katika Nyumba ...................................................... 80

Majukumu ya Wanawake – Kazi za Kufanya ..................................... 93

**Mpango wa Mungu wa Wokovu** ............................................... 106

# Wajibu wa Wanaume:

## Katika Kanisa

## Katika Uongozi

## Katika Nyumba

Louis Rushmore

# Uongzi wa Kiume katika Kanisa

## Utangulizi

Ni jambo la muhimu sana kufafanua misingi ya Biblia, na hasa pale inapotofautiana na dini (madhehebu) ya kisasa. Kwa sababu makanisa ya Kristo ni mali ya Kristo (Warumi 16: 16), yanawajibika kujiendesha sawasawa na anavyoagiza (Wakolosai 3: 17). Kwa kweli, watu wote wanaoishi nyakati za Injili wanapaswa kushika maneno ya Yesu Kristo kuliko ya Musa au ya Manabii wa Agano la Kale (Mathayo 17:1-5; Yohana 12:48). Zaidi ya yote, Yesu Kristo ni mtoa sheria (Yakobo 4:12) na Mpatanishi (Waebrania 9: 15) wa Agano Jipya, ambalo kwalo watu wanaoishi leo, lazima waligeukie ili kupata maelekezo ya kidini au ya kiimani. Na kwa nyongeza Yesu Kristo **alilaani** kitendo cha cha kubadili maagizo au sheria ya Mungu na kushika ***"maagizo ya wanadamu" (***Mathayo 15:9). Mtume Paulo, akijaa Roho, pia **alilaani *"Injili za namna nyingine"*** (Wagalatia 1:6-9) na kushika mapenzi ya wanadamu badala ya mapenzi ya Mungu (Wakolosai 2:23). Kwa hiyo, mtu anapaswa kuigeukia Injili peke yake ili ajifunze kile ambacho Mungu alichoidhinisha katika Ukristo.

Wajibu wa Wanaume na wanawake ndani ya Kanisa na huko nyumbani, hauko kimila, bali unarudi nyuma katika uumbaji. Ulianzishwa na Mungu kabla ya kuwepo mila yoyote (1 Timotheo 2:13-14; 1 Wakorinto 11: 8-9).

Makanisa ya Kristo, yanawajibika kuanzisha katika makusanyiko yao, aina ya uongozi wa kanisa ambao Agano jipya linauruhusu. **Kwa hiyo, makanisa ya Kristo hayana uongozi wa Wanawake ndani ya Kanisa, kwa sababu, haujaruhusiwa na Mungu.** Kwa kuwa Mungu amewazuia wanawake kuwa kwenye majukumu ya uongozi ndani ya

Kanisa, hii inaweka wajibu huu kwa waumini wa kiume kuchukua wajibu huu waliopewa na Mungu (1 Timotheo 2:8).

Kila mmoja anayeheshimu mamlaka ya Biblia, na anayependa kumpendeza Mungu atajihusisha na **Kile ambacho mwenyezi Mungu amekiidhinisha**. Kwa upande wa uongozi wa kanisa, hii ina maana kwamba Kanisa hilo litaongozwa na watu wenye hofu ya Mungu, na kwamba kanisa halitakuwa na viongozi wanawake. Hatuwezi kubadilisha wajibu ambao Mungu amewapa wanaume na wanawake kama ambavyo hatuwezi kubadilisha mpango wa Mungu wa wokovu. Kuharibu kwa namna yoyote ile maagizo au sheria za Maandiko, kunaweza kukawa na madhara kiroho na tena kwa umilele!

## Kumomonyoka Kwa Uongozi wa Kiume

Tabia ndani ya jamii za kisasa duniani kote, tayari zimekiuka ule wajibu ambao Mungu alitoa kwa wanaume na wanawake. Wanawake sio duni kabisa kwa wanaume kwa akili na pia kiroho. Lakini pia usawa kati ya wanaume na wanawake kiroho ni fundisho la kibiblia (Wagalatia 3:27-28). Na kwa nyongeza, usawa kati ya wanawake na wanaume katika sehemu za kazi unaweza kushinda, na nadhani hii ni sawa tu. Lakini ndani ya nyumba au nyumbani na kanisani, Mungu mwenyewe ameweka wazi majukumu ya mwanamke na mwanaume, na Wakristo waaminifu hawapaswi kutoka kwenye maagizo hayo ya Mungu. Sababu ya kwamba kwa miaka zaidi ya 6,000 wanawake wamekuwa wakiwatii Wanaume, nyumbani na katika dini, ni kwa sababu Mungu aliweka fundisho hilo katika Maandiko matakatifu. Kwa karibu miaka 2,000 iliyopita Mungu amelijumuisha katika Agano Jipya, kwamba wanawake wawatii wanaume huko nyumbani na katika kanisa. Licha ya **usahihi wa kisiasa**, katika jamii za kisasa, pengine hakuna kitu kizuri kinachoelezea wajibu usiobadilika kwa wanaume na

wanawake, kama Mungu alivyopanga ukweli usiobadilika unabaki kwamba wanawake wa kizazi chetu bado watalazimika kuzaa uzao wetu (wanaume). Mtume Paulo alisema juu ya wajibu huu, katika 1 Timotheo 2: 15. ***Wajibu wa mwanamke katika kanisa au ndani ya nyumba*** una utata tu kwa wale ambao hawaheshimu mamlaka ya Mungu na neno lake.

Neno la Mungu lililovuviwa, linatoa sababu kadhaa za wanawake kuwa chini; (1) Adamu aliumbwa kwanza, halafu Hawa (1 Timotheo 2: 13); (2) Ni mwanamke, sio mwanaume aliyedanganywa na Shetani (1 Timotheo 2: 14); (3) Mwanamke aliumbwa kutoka katika mwanaume (1 Wakorintho 11: 8); (4) Mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanaume (1 Wakorintho 11:9). Pamoja na hivyo, wokovu wa mwanamke na thamani yake havimtegemei mwanaume (Wagalatia 3:28). Injilihaibagui utofauti baina ya rangi, siasa, hali ya kiuchumi, au jinsia. Kipimo cha Wakristo, ikiwa ni pamoja na wanawake, sio matendo ya jamii inayowazunguka (Warumi 12: 2). Mamlaka ya mwisho juu ya mwenendo wa wanaume na wanawake Wakristo, iwe nyumbani au kanisani, uko mikononi mwa Mungu. Baba yetu wa mbinguni ana **haki** ya kutenganisha kati ya wajibu wa wanawake na wanaume.

## Hapo Mwanzo

Uongozi wa Wanaume ndani ya kanisa alilojenga Yesu, una chanzo chake katika bustani ya Edeni. Naam, miaka 4,000 kabla ya kuanzishwa Kanisa la Agano Jipya, Mungu mwenyezi alianzisha uongozi wa wanaume katika dini na hata nyumbani. Msingi huu wa uongozi wa Wanaume uliendelea kwa kipindi chote cha mababa na kile cha Torati, na uongozi wa wanaume umeendelea kuwepo kwenye Ukristo.

Tunachokijadili hapa hasa ni "Wajibu wa Wanaume", isipokuwa msisitizo wetu hasa unahusu uongozi wa wanaume ndani ya Kanisa.

Akiwa amevuviwa, Musa aliandika juu ya matokeo ya dhambi katika bustani ya Edeni, ***"Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala"*** (Mwanzo 3:16). Kwa hiyo, wajibu wa kutii wa mwanamke kwa mwanaume, hautokani na mila au tamaduni, lakini wajibu huo ulikuwepo kabla ya vyote hivyo. Pia Injili, haikubadilisha wala kuondoa wajibu wa mwanamke wa kutii, wala haikuondoa; (1) Kuzaa kwa utungu (2) kula kwa jasho (3) kifo cha kimwili. Vyote hivyo vitakuwepo mpaka mwisho wa nyakati.

Akiwa amevuviwa, mtume Paulo aliunganisha uongozi wa wanaume ndani ya kanisa na uongozi wa mwanaume katika bustani ya Edeni. ***"Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa"*** (1 Timotheo 2:11-14). Vile vile akiliandikia Kanisa la Korintho, mtume alionyesha fundisho hilo hilo. ***"Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanaume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanaume, na kichwa cha Kristo ni Mungu…wala mwanaume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, ila mwanamke kwa ajili ya mwanaume"*** (1 Wakorintho 11:3, 9). Haifai kwa mwanamke kujichukulia wajibu ambao Mungu aliukusudia kwa mwanaume, kama ambavyo pia sio sahihi kwa mwanaume kujichukulia wajibu ambao ni wa Yesu Kristo. Kwa hiyo, Wadada Wakristo, wasithubutu kufundisha wanaume katika jumuiya, na wanaume

Wakristo hawana ruhusa ya Mungu kuwaruhusu wamama wafundishe wanaume kanisani kuhusiana na dini. Kwa kadiri Mungu na wana wa Mungu wanavyohusika, wajibu uliotolewa na Mungu kwa wanawake na wannaume, hauathiriwi na mila za jamii za kisasa.

## Wajibu wa Wanawake Unafafabua Wajibu wa Wanaume

Wajibu wa wanawake unasaidia kuelezea "wajibu wa wanaume" hususani, wajibu wowote ambao **sio wa mwanamke**, lazima utakuwa ni **wajibu wa mwanaume.** Kwa mfano, katika Agano Jipya wanawake wamekatazwa kufundisha wanaume mambo ya dini. ***"Mwanamke na ajifunze kwa utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwannamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanaume, bali awe katika utulivu"*** (1 Timotheo 2: 11, 12). ***"Wanawake na wanyamaze katika Kanisa, maana hawana ruhusa ya kunena bali watii, kama vile inenavyo Torati nayo. Na kama wakitaka kujifunza neno lolote na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao, maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa"*** (1 Wakorintho 14:34-35). Kwa hiyo, wanaume wanawajibika kufundisha Neno la Bwana kwa watu wote. Hata hivyo, Akila na Prisila, Wakristo ambao ni mume na mke, wanaonyesha kwamba, mwanamke anaweza kumfundisha mwanamume wakiwa peke yao (Matendo 18:2426), ikiwa hatachukua mamlaka juu yake, au kufundisha katika namna ya kumtawala (1 Timotheo 2:12). Wanawake Wakristo, lazima wawafundishe waume zao wasio Wakristo (1 Petro 3:1), lakini kwa mfano ikiwa wanaume hao hawatazingatia maneno yao. Wanawake pia wananena na kufundisha, pale wanaposhiriki katika kuimba (Waefeso 5:19; Wakolosai 3:16). Vinginevyo wanawake wamekatazwa na Maandiko Matakatifu kuhubiri au kufundisha wanaume hadharani.

## Agano Jipya Linafafanua Wajibu wa Wanaume katika Kanisa

**“**Wajibu wa wanaume” katika kanisa la Bwana umewekwa na Bwana, na haupo pale ili kubadilishwa au kuachwa na Wakristo wanaume. Kabla mtu hata hajaanzisha mjadala juu ya viongozi wa kanisa (yaani, maaskofu, mashemasi, wahubiri, na waalimu), wanaume Wakristo (na wanawake), lazima watambue kwamba, Mungu amewachagua wanaume dhidi ya wanawake kuliongoza kanisa.

Katika kanisa, wajibu wa uongozi wamepewa wanaume, na huduma saidizi, wamepewa wanawake. Lakini bado, si kila mwanaume anaweza kuwa askofu (1 Timotheo 3:1-7), shemasi (1 Timotheo 3:8-13), mhubiri au mwalimu (1 Wakorintho 12:18). Hata hivyo, wanaume kwa ujumla, wanaamrishwa na Mungu kubeba majukumu ya kuelekeza, na kufundisha kanisani. Mungu amekataza wanawake kubeba majukumu haya.

Kwamba wanaume na sio wanawake, ndio wanaopaswa kuongoza kanisa, hilo liko wazi katika mafundisho ya Agano Jipya, kwamba wanaume ndio waongoze sala ya wote. ***“Basi nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano”*** (1 Timothy 2:8). Neno “wanaume” lina maana ya, “jinsia ya kiume”. Kwa nyongeza tu, “wanaume” katika mstari wa 8, linatenganishwa na “wanawake” katika mstari wa 9.

## Hitimisho

Hakuna anayeweza kuthubutu kubadilisha fundisho lolote la Agano Jipya (Wagalatia 1:6-9; Ufunuo 22:18-19). Naam na hasa, Wakristo lazima wawe waangalifu kushika wajibu na majukumu yao ya wanaume na wanawake ndani ya kanisa, ambayo yameamriwa na

Mungu mwenyewe. Ukweli kwamba wanaume wengi wanaweza wasijitokeze kwenye mchakato wa kuchagua waalimu au wahubiri, ni habari mbaya kwa wanaume, hata hivyo, udhaifu huo wa kibinadamu haubadilishi sheria ya Mungu kuhusu majukumu ya wanaume na wanawake ndani ya kanisa. Ukweli ni kwamba wanaume wengi wanaweza wasiibuke katika nafasi ya kuwa mume na baba nyumbani kama wanavyopaswa kuwa, hata hivyo, udhaifu huo wa kibinadamu haumfanyi, kwa mfano, mke kuwa mume, au mama kuwa baba. Nyumbani yanahitajika majukumu yote ya mke na mume ili kuwepo na ushirikiano ambao Mungu alikusudia uwepo. Kadhalika kanisa linahitaji majukumu yote ya wanawake na ya wanaume ili liwe kanisa lenye ushirikiano, kama Mungu alivyokusudia.

Pindi wanawake Wakristo wanapochukua majukumu ya wanaume, iwe nyumbani au Kanisani, ni kosa la Wakristo wanaume. Ingawa wanawake pia watalaumika. **Kwanza**, wanaume wanapaswa kuchukua majukumu kanisani na nyumbani, ambayo Mungu amewapa. **Pili**, Wakristo wanaume, wanatakiwa wawakataze, Wakristo wanawake, wasichukue majukumu ambayo Mungu hakuwapa. Majukumu yale yale katika dini na hata nyumbani, ambayo Mungu aliyaanzisha tangu binadamu alipoanza safari ya maisha hapa duniani, bado yanaendelea (hayajabadilika). Kwa muundo wa ki-mbingu, jukumu la shughuli za mkutano wa kanisa, wamepewa kipekee wanaume wateule.

# Uongozi wa Kiume katika Uaskofu

## Utangulizi

Kanisa la Kristo la kwanza lilikuwa Yerusalemu, mitume wa Kristo waliliongoza kanisa hilo, lakini kwa wakati ambao haukusemwa, maaskofu walichaguliwa katika kusanyiko la Yerusalemu (Matendo 11:30; 15:2; 16:4). Ukristo ulienea tokea Yerusalemu kwenda duniani kote (Matendo 1:8; Marko 16:15; Wakolosai 1:23). Maaskofu bila shaka walikuwa ni sehemu muhimu ya kufundisha Injili na kueneza Ukristo duniani kote.

> Wazee ni sehemu ya mpango wa Mungu kwa Kanisa. Kanisa la Yerusalemu lilikuwa na wazee (Matendo 15:46). Paulo aliweka maaskofu katika kila kanisa, wakati anarudi toka safari zake za umisionari (Matendo 14:23). Kanisa la Efeso lilikuwa na wazee (Matendo 20:17). Kanisa la Filipi, ambalo wakati mwingine liliitwa kanisa la mfano, lilikuwa na maaskofu (Wafilipi 1:1). Paulo alimwacha Tito Krete, ili ***"aweke wazee katika kila mji"*** (Tito 1:5). Petro aliwasihi maaskofu, ***"walio kwenu"*** (1 Petro 5:1). Wazee wanawekwa na Roho Mtakatifu wanapotimiza vigezo vilivyofunuliwa na Yeye (na kuchaguliwa na kusanyiko husika); ***"ambalo Roho Mtakatifu amewaweka…kuwa waangalizi"*** (Matendo 20: 28) (Goug 9).

Kuchagua wazee katika kanisa ni fundisho muhimu la Biblia. Na zaidi, jambo hili linahitaji umakini mkubwa na kuwajibika, kwa kila kanisa. "Mtume Paulo alimuagiza Tito kuweka wazee katika kila mji huko Krete (Tito 1: 5). Kuchagua watu sahihi kwa kazi hii kubwa ilikuwa

ni jambo muhimu. Hivyo, Paulo anatoa orodha ya sifa ambazo watu hawa walipaswa kuwa nazo kwa wakati ule wanapochaguliwa kwenye nafasi hii ya kiroho katika kanisa la Bwana" (Stevens). "Hakuna kusanyiko linaloweza kuweka uangalifu mkubwa katika kuchagua waangalizi wake wa kiroho. Watu hawa, watakapokuwa wamechaguliwa, ama wataongoza kanisa kwa viwango vya juu vya utumishi wa Yesu Kristo, au wataliongoza kanisa kwenye kupoa, kwenye uvuguvugu, kwenye mkwamo wa kiroho na hatimye kwenye kifo cha kiroho" (Taylor 87).

"Kwa mara ya kwanza kutajwa kuwa tuna wazee ndani ya kanisa ni katika Matendo ya Mitume 11:30" (Boles, *Makanisa ya Kristo uk. 9*). Kila kanisa la Bwana, lenye uongozi kamili, linaongozwa na wazee waliochaguliwa kwa vigezo vya kibiblia (1 Timotheo 3:1-7; Tito 1:5-9). Hata hivyo, ni kwa namna gani kanisa lisilo na wazee linapaswa kuongozwa? Je, mhubiri anaweza kuongoza kanisa pasipo wazee? Je, inakubalika kibiblia kuchagua kamati kuongoza kanisa? Je, wadhamini wanapaswa kuongoza kanisa? Je, mtunza fedha anayo mamlaka kuamua juu ya kanisa? Je, kura ya wengi, wanaume kwa wanawake, inaweza kuamua kwa niaba ya kanisa? Je, wanaume waaminifu wanawajibika kuamua mambo ya kanisa? Kimaandiko ni nani anayepaswa kuongoza utendaji wa kanisa ambalo halina wazee?

Je, kanisa linaweza kuwepo bila wazee? Ndiyo, ni wazi kwamba makanisa katika karne ya kwanza, **yalikuwepo** kwa muda fulani kabla ya kuweka wazee (Tito 1:5). Na hii ni wazi kwamba kwa muda **yalitenda kazi** bila wazee. Hata hivyo, baadaye makanisa haya yalikua kwa kiwango ambacho wazee walichaguliwa. Bado swali linabakia, hata hivyo, "Ni kwa jinsi gani kanisa lisilo na wazee linapaswa kujiendesha?"

# Bado Hakuna Wazee!

Jambo linaloitwa "**uongozi wa kiinjilisti**" sio jawabu la uongozi wa kanisa lisilo na wazee. Mungu alipanga uongozi ujumuishe wingi wa wanaume, ambapo inashauriwa kwamba, asiwepo mtu mmoja, licha ya wema wake au sifa za kipekee alizo nazo, anayefaa kwa kazi kama hiyo. Mhubiri sio bosi, na asijiruhusu kuwa mtu anayefanya maamuzi ya kila siku (*mpaka kanisa litakapomwondoa kazini*). Badala yake, mapema iwezekanavyo, mhubiri au mtumishi, au mwinjilisti, anapaswa kuwaongoza watu wa kanisa wakue kiroho. Mhubiri anatakiwa kuwawezesha na kuwafundisha wanaume kushika maeneo ya uwajibikaji na utumishi hata kama anaweza kuyafanya vizuri yeye mwenyewe. Mhubiri anatakiwa kulifundisha kundi kana kwamba yeye anataka kuacha kazi. Hata hivyo, kwa kweli, daima kutakuwa na mengi ya kufanya kwa mtumishi wa Mungu atumikaye kuliko awezayo kufanikisha katika maisha yote.

**Kamati** sio njia mbadala nzuri ya uongozi wa kanisa badala ya wazee. Kundi pekee la wanaume ambalo idadi yake ni ndogo kuliko wanaume wote wa kanisa hilo, walioruhusiwa na Maandiko kutawala kusanyiko husika, ni wazee. Wakati fulani wahubiri au wanaume wengine washirika wanakosa shauku ya kuweka uongozi wenye sifa za kibiblia kwa sababu wanajua kwamba hawawezi kuwa na sifa za kimaandiko za kutumika katika uaskofu. Hususani wanaume wabinafsi wasioweza kutumika kama wazee wanajua kwamba ushawishi wao na uwezo wao wa kupitisha maamuzi yao hautakuwepo tena pindi uongozi utakapowekwa katika kusanyiko.

**Wadhamini** wanaotambulika kisheria sio njia inayokubalika kwa kuongoza kanisa pasipo wazee. Ingekuwa kwamba sio takwa la kisheria la serikali kwamba makanisa yawe na wadhamini, makanisa ya Kristo yasingekuwa na wadhamini kabisa, kwa sabbabu hawatajwi katika

Agano Jipya. Kwa hiyo, majukumu ya wadhamini hasa yako kimwili na sio katika mambo ya kiroho. Suala ni kwamba, pale sheria ya nchi inapotaka wadhamini au jamaina fulani ya uongozi kama huo, wazee wa kanisa hilo wanapaswa kuhudumu katika jukumu hilo. Kwa njia hiyo sheria ya Mungu na sheria ya binadamu zitakuwa sambamba.

**Mweka hazina,** lazima awe makini ili asitumie nafasi yake (ya utumishi) kwa kujaribu kuliongoza kanisa. Wakati mzee anaweza kuwa mweka hazina, mweka hazina (hata kama ni mtu mzima) hatakuwa sawa na wingi wa wanaume, wanaotumika kama wazee. Zaidi sana akionyesha tabia, iwe kwa maneno au kwa matendo kwamba mweka hazina anayelitawala kusanyiko kwa kufanya maamuzi ya lini fedha itoke ni dhambi na si utauwa (3 Yohana 9-10).

**Kura ya kanisa,** ambapo wanawake na wanaume wanaamua mambo ya kanisa inakiuka heshima ya majukumu ya wanaume na wanawake juu ya mambo ya kiroho (1 Timotheo 2:12-14). Kama ilivyo hata nyumbani (Waefeso 5:22-24; Mwanzo 3:16), vivyo hivyo katika kanisa (1 Wakorintho 11:8-9), Biblia inafundisha wanawake watii mamlaka ya wanaume. Kwa uwazi kabisa, waumini wa kiume wanao wajibu wa kuelekeza, kutenda na kuamua juu ya kanisa panapokuwa hakuna wazee. Itakapokuwa imewekwa vizuri, na kuchaguliwa kundila wanaume wenye sifa (Uongozi) wana wajibu huu katika kila kusanyiko husika. Waumini wote wanaume watu wazima wa kusanyiko lisilo na wazee wanatakiwa kushirikiana kwa ajili ya uendeshaji wa kanisa husika. Halafu, kutoka miongoni mwao wana wajibu wa kuchagua watu wenye sifa za kibiblia ili wawe wachungaji.

## Wazee Wanahitajika

Wakati mwingine kusanyiko linaweza lisiwe na maaskofu kwa kipindi fulani huko nyuma, kwa kuwa hakukuwa na wanaume wawili au

zaidi wenye sifa kibiblia, waliokuwa tayari kutumika kama wazee na watu ambao kanisa linawaheshimu vya kutosha ili wawaongoze. Sifa za kibiblia katika 1 Timotheo 3:1-7 na Tito 1:5-9, zote zinajumuisha wanaume fulani Wakristo na kuwaengua wanaume wengine Wakristo katika mchakato wa kuweka wazee. Pamoja na hayo, pindi wanaume wawili au zaidi wanapokidhi sifa za kibiblia za kuchaguliwa kuwa wazee, inaonesha mpango mtakatifu wa Mungu wa uongozi wa kusanyiko ni ili kanisa liwe na maaskofu.

Angalia Tito 1:5; ***"Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru"***. Kwa uvuvio mtume Paulo alilirejelea kusanyiko lisilo na wazee kama "linalohitaji" au "linalopungukiwa". Neno hilo hilo la Kigiriki lililotafsiriwa kama, kuhitaji au kupungukiwa, katika (Tito 1:5) linatokea pia katika (Luka 18:22) kama "kupungukiwa", na tena katika Yakobo 1:5 kama "kukosa" na "fukara" katika Yakobo 2:15. Angalia upya kila moja ya aya hizi na uamue kama, "upungufu" au "uhitaji" na "umaskini" ni kitu cha kuzingatia. ***"Yesu aliposikia hayo alimwambia, umepungukiwa na neno moja bado; viuze ulivyo navyo vyote, ukawagawanyie maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuate"*** (Luka 18:22), ***"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa"*** (Yakobo 1:5). ***"Ikiwa ndugu ndugu mwanamume au mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki"*** (Yakobo 2:15). Naam, kinachojalisha ni "kuhitaji", "mapungufu" au "kupungukiwa," na "ufukara".

Wasomi na waandishi; Barnes, Poole na *Wycliffe,* wanalinganisha uhitaji katika Tio 1: 5, kama kitu "kilichoachwa bila kufanyika" kwa habari ya kuweka wazee. Mwandishi mwingine, Adam Clarke, anatumia neno "udhaifu" kuelezea kusanyiko lisilo na wazee.

Mwandishi mwingine, Matthew Henry, anaondoa uwezekano wa kuweka wazee kama suala la hiari: anasema "Palipo na idadi ya kutosha ya waumini, wazee lazima wawekwe; mwendelezo wao katika makanisa ni walazima…" Kadhalika, ilikuwa ni utaratibu wa mtume Paulo kuweka wazee katika kila kusanyiko alilolianzisha. ***"Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini"*** (Matendo 14:23). "Hakuna hoja hata moja iliyotolewa kupinga uwekaji wa wazee wenye sifa katika kila kanisa ambayo itasimama dhidi ya neno la Mungu" (Phillips 275).

Kila kusanyiko lililosimama vizuri litakuwa na wazee wenye sifa za kibiblia wakitumika kama waangalizi juu yake (Matenndo 20:28). Kusanyiko lolote ambalo halina wazee halijakamilika vikamilifu kulingana na Ukristo unaotokana na Agano Jipya. Ingawa sifa za wazee kibiblia hazipaswi kuchukuliwa kwa wepesi, inawezekana zikaeleweka vibata, kwa kuzifanya ngumu sana kiasi kwamba hakuna mwenye mwili anayeweza kufuzu kuwa askofu. Mungu alipanga kila kusanyiko katika makanisa ya Kristo liongozwe na maaskofu ambao nao wanawajibika kwa Mungu, kwa kila roho ndani ya kanisa (Waebrania 13:17). Yesu Kristo ni Mchungaji Mkuu na chini yake wachungaji au wazee wanatumika (1 Petro 5:1-4). Hiyo ni sheria ya Mungu na ni kitu cha kufanya kwa ustawi wa Kanisa lolote.

## Sifa za Wazee Kibiblia

Mungu hakuliacha kanisa bila mwongozo unaofaa katika dini. Yesu Kristo ndiye kichwa cha kanisa ambalo alilifia (Waefeso 5:23-25). Neno la Mungu ndiyo mamlaka ambayo tunapaswa kuiendea, kwalo tunalazimika kuishi, na ambalo kwalo tutahukumiwa siku moja (Mathayo 28:18-20; Luka :4; Ufunuo 20: 11-15). Wazee (ambao pia

wameitwa katika Biblia kama maaskofu, wachungaji, waangalizi) wana **mamlaka** ya Kristo, na wana **wajibu** wa kuliongoza kanisa ambalo wanalichunga (Matendo 20: 28). Wazee wana wajibu mkubwa duniani, ambao ni kuchunga roho za wengine (Waebrania 13:17). Matokeo yake, Agano Jipya lina sifa ambazo lazima zitimizwe na wazee husika (1 Timotheo 3:1-7; Tito 1:5-9). Hata majina ambayo Agano Jipya linatumia, yanaonyesha mambo fulani juu ya sifa zao na kazi zao.

Hata hivyo, sifa za wazee ziko namna hiyo ili kila Mkristo, mwanaume na mwanamke anapaswa kujitahidi awe nazo pia. Isipokuwa kwa sifa ***"awe mume wa mke mmoja"*** wanawake hawawezi kuwa nayo***.*** Bila shaka, Wakristo wanaume na wanawake pia wanaweza kuamua kubaki bila kuoa au kuolewa kama mtume Paulo alivyofanya. Vinginevyo, ingawa sifa zinazotakiwa kwa wazee zinapaswa kuwa ndio lengo na kila mwana wa Mungu kuwa nazo pia. Hata hivyo, maadili haya ambayo ni kwa ajili ya kila mwana wa Mungu ni lazima kwa Wakristo wanaume wawe nazo tayari wanapochaguliwa kuwa wazee.

> Zipo sifa chache zilizoorodheshwa kwa ajili ya wazee, ambazo hazina ulazima kwa Wakrito wengine. Sifa zilizotajwa zinapaswa kuwa kwa kila mwanaume. Kwa nini ndugu asishuhudiwe mema na watu wa nje ya kanisa? Kwa nini asiishi kiasi kwamba wale wasiokubali dini ya Ukristo, waone wema katika tabia zake? Kwa nini asifae kufundisha, mpole, asiyelaumika, mtakatifu, mwenye haki anayempenda Mungu, mvumilivu, mkaribishaji, asiyezoelea ulevi, mwangalifu, na mume au baba mzuri? Kwa nini kila ndugu asidhiti mihemko yake, kutoa hukumu kwa wengine, kuwa mtu wa amani, kuepuka tamaa, na kutokutumia vileo? Hakuna sifa ya wazee isiyowezekana (Boles, *"Qualification"* uk 30).

Mara nyingi kuna mkanganyo kuhusu wazee (na majina yao mengine) kwa sababu Biblia inavyowaelezea ni tofauti sana na jinsi wanavyotumika katika madhehebu. Madhehebu moja inawaita wazee vijana wasiooa bado, wanaenda nyumba kwa nyumba, wawili wawili, kuhamasisha fundisho hilo la madhehebu. Hata hivyo, kwa mujibu wa Biblia, wazee wameoa! Mtindo mwingine wa kidini wa kutungwa na wanadamu askofu asiyeoa hutawala eneo kubwa kijiografia (makanisa mengi). Lakini kwa mujibu wa Biblia askofu anatawala kusanyiko moja tu, na ni mwanaume aliyeoa. Madhehebu mengi yanalinganisha mhubiri na mchungaji, ambapo Agano Jipya halifanyi huo ulinganifu. Badala yake neno la Mungu linatumia jina "wachungaji" sawa sawa na jina "wazee". Kuliko kushiriki katika mkanganyiko wa kimadhehebu, tunahitaji kugeukia Agano Jipya kwa uelewa sahihi wa maneno ya Biblia; wazee, maaskofu, waangalizi, na wachungaji, Agano Jipya linatumia majina mbali mbali kwenye ofisi ya wazee. Neno mzee limetafsiriwa kutoka katika Kiyunani, *Presbuteros*. Hata hivyo, neno linalotafsiriwa mzee lina maana ya mwenye umri mkubwa. Neno hili linatokea mara 69 katika Agano Jipya; mara 19 likimaanisha wazee wa kanisa (cheo), mara 34 likimaanisha wazee wa Kiyahudi, mara 4 likimaanisha umri, na mara 12 likimaanisha wazee wa Mbinguni katika Ufunuo. Mifano ya wazee wa kanisa la Agano Jipya ni pamoja na; Matendo 11:30; 14:23; 15:2, 4, 22-23; 16: 4; 20:17; 21:18; 1 Timotheo 5:17, 19; Tito 1:5 na Yakobo 5:14.

Maneno "askofu" na "mwangalizi" yametafsiriwa toka katika neno la Kiyunani *episkopos*. Neno lina maanisha mkaguzi, mwangalizi, mlinzi, au mtu aliyewekwa kusimamia vitu vinavyofanywa na wenngine vifanyike sawa sawa, kuwa na mamlaka, kulinda roho, au mtu anayeangalia mambo ya wengine. Neno hili la Kigiriki linaelezea majukumu au aina ya kzi. *Episkopos*, linatafsiriwa kama askofu au

maaskofu, likirejelea wazee ndani ya kanisa katika 1 Timotheo 3:1-2; Tito 1:7 na Wafilipi 1:1. Limetumika kumaanisha Yesu Kristo katika 1 Petro 2:25. *Episkopos*, limetafsiriwa kama mwangalizi katika Matenddo 20:28.

Neno “wachungaji” limetafsiriwa kutoka neno la Kigiriki, *Poiman*. Likimanisha mchungaji wa mifugo, mchungaji, meneja, mwongozaji au msimamizi. Neno hili linamaanisha kuchunga kwa upole, kwa upendo, kwa umakini na kwa uangalifu mkubwa. Neno hili limetumiwa sana kwa wachungaji wa kondoo (Luka 2:8). *Poiman* limetafsiriwa mara moja tu kama “mchungaji” likimaanisha ofisi ya uchungaji katika Waefeso 4:11. Vinginevyo (nje ya Injili) linatafsiriwa kama “mchungaji” na kutumika kwa Yesu Kristo, Mchungaji mkuu (Mathayo 25:32; Yohana 10:11, 14, 16; Waebrania 13:20) ambaye chini yake wapo wachungaji wakimsaidia (1 Petro 2:25).

Sasa kwa kuwa tumefahamu majina ya kibiblia ya hawa wazee, sasa tunahitaji kuangalia kwa ukaribu sifa za kibiblia ambazo mwanaume Mkristo lazima awe nazo ili aweze kuchaguliwa na kusimikwa kuwa mchungaji. Sifa hizo zinaonekana sehemu mbili tu katika Agano Jipya; 1 Timotheo 3:1-7 na Tito 1:5-9. “Sifa hizo zinagawanywa katia makundi sita ya asili…. Zinatofautishwa kulingana na uzoefu, heshima, uhusiano wa ndani, tabia, uwezo wa kufundisha na kutawala” (McGarvey uk. 53).

## “Mtu Akitaka Kazi ya Askofu, Atamani Kazi Njema”

(1 Timotheo 3: 1)

Moja ya matakwa katika sifa za wazee ni kwamba mtu “atamani” na “sio kwa lazima, bali kwa hiari” (1 Petro 5:2) achukue wajibu wa kuwa mmoja wa wachungaji wa Mungu. “Uaskofu huu sio

kwa watu ambao wanalazimishwa kuupokea, na kuendelea kulazimishwa kushikilia nafasi hiyo" (Taylor 86). "Shauku ya ndugu ya kuhitaji kuhudumu kama mchungaji wa kundi la Mungu, lazima iwe ni sahihi. … Hakuna mtu anayefaa kuhudumu kama mzee wakati lengo la kufanya hivyo ni kujitukuza kwa watu wanaomzunguka…" (Campbell 20). "Kutamani" kunahitajika kutoka katika upendo thabiti wa fursa ya kutumikia kanisa la Bwana.

Neno lililotumika kama "Ofisi" (KJV) au "nafasi" (NKJV) lina maana ya "kazi". Kuwa mzee sio ofisi ya kifahari kwa jinsi ilivyo katika eneo la utumishi au kazi ya Ukristo.

## "Basi Imempasa Askofu Awe…"

(1 Timotheo 3:2)

Neno "awe" linatangulia sifa zote, ambazo mtu anatakiwa kuwa nazo kabla hajawa mtu anayefaa kuteuliwa kuwa mzee. Ni wazi kwamba, dhambi inayoendelea, au kutojutia dhambi katika maisha ya mzee kunaweza kumfanya akose sifa za kuendelea kama mmoja wa wachungaji wa Mungu. Hata hivyo, baadhi ya sifa anazozitaka Mungu kwa wazee, sio lazima ziwe za kuendelea. Je, mtoto anapokua na kutoka nyumbani, kunamnyima sifa ya kusimamia nyumba yake vema? Au kifo cha mke wa mchungaji, kinaondoa ukomavu na uzoefu alioupata katika maisha ya ndoa?

> Mtume Paulo anamaanisha kwamba, kama akipatikana mtu mwenye sifa, basi mtu huyo ateuliwe kama mzee au askofu. Mtu huyo anayeteuliwa lazima awe na sifa, "**wakati ule anapoteuliwa**". Hii inaonyeshwa na matumizi ya kauli hizi, kwa maana ya wakati uliopo,…mara nyingi, wakati uliopo unapotumika, mtu anaweza kusema, "hilo ni tendo

> linaloendelea kwa nyakati zijazo (kutegemea na aina ya wakati uliopo uliotumika), haipo hivyo mara zote…Kwanza haitoshi kutambua kitenzi, cha wakati uliopo tu. Lazima tuulize, hiki ni aina gani ya kitenzi cha wakati uliopo? Pili; maana ya kitenzi na jinsi kilivyotumika ni muhimu sana.…wakati uliopo, unaoendelea, unaonyesha tendo linaendelea katika wakati uliopo. (Stevens)

Neno "kuwa" katika Kiyunani, na hata katika Kiingereza ni kitenzi kinachounganisha, au kitenzi cha kuwa. Neno la aina hii linaelezea tendo linaloendelea kwa wakati uliopo. Neno "kuwa" katika Tito 1:6, halielezei mazingira kabla au baada ya muda ambao wema wa mtu unaangaliwa kuhusu uwezekano wa kuchaguliwa kuwa Mzee. Uelewa huu unaunganika moja kwa moja na tafsiri sahihi ya vifungu kuhusu sifa za wazee.

> Kwa sababu kitenzi hiki kipo katika hali ya taarifa, tunajua kwamba kinatupa picha ya **tendo linaloendelea katika wakati uliopo**. Kwa nini jambo hili ni la muhimu sana? Huwezi kutumia kitenzi cha wakati uliopo katika Tito 1:6, kuthibitisha kuwa, miaka 20 au 30, **baadaye mtu qlichaguliwa kuwa mzee**, lazima ajiuzulu kama mke wake atakufa. Au watoto wake wakifa katika ajali ya gari, lazima ajiuzulu kwa sababu hana watoto wanaoamini. Au kwamba kama watoto wake wakubwa wakianguka amekosa sifa kwa kitendo hicho na lazima ajiuzulu kuwa mzee. Mzee anaweza kujiuzulu katika mazingira kama hayo, lakini halazimiki kufanya kwa kigezo cha kitenzi cha wakati uliopo katika Tito 1:6. (Stevens)

## “Asiyelaumika”

(1 Timotheo 3:2; Tito 1:6)

“Asiyelaumika” maana yake asiye na mashitaka, asiyekubalika, ambaye hana lawama. Hata hivyo, “asiyelaumika” haimanishi mkamilifu asiye na dhambi. Kwa mtazamo wa binadamu, wazee wanaweza kuonekana wakamilifu wanapolinganishwa na watu wengine, lakini sio kwamba hawana dhambi muda wote wa maisha yao. Asiyelaumika, maana yake ni kutostahili kukemewa na jamii, raia mwema katika jamii na katika kanisa. Mzee huyo haonyeshi tabia zisizofaa (Jackson 29). Sifa zifuatazo za askofu zinaweza kuelezea nini maana yake mtu kuwa “asiyelaumika”. “Uaskofu ni nafasi ya kazi na ulimwengu wa shughuli unaohitaji watu wanaoheshimika, waadilifu na wanyoofu” (Taylor 68).

## “Mume wa Mke Mmoja”

(1 Timotheo 3:2; Tito 1:6)

Matendo ya wapagani na hata wana wa Mungu (1 Samweli 1:2; 2 Samweli 3:2-5; 5:13) katika historia, mara nyingine yalijumuisha kuoa wake wengi. Mtume Paulo alimtaarifu Timotheo kwamba mtu mwenye mke zaidi ya mmoja hakustahili kuchaguliwa kuwa mzee. Mume wa mke mmoja, kwa tafsiri ya kawaida ina maana ya mke mmoja kwa wakati mmoja au asiwe na wake wengi, na kwa nyongeza ya maana ya kawaida ya aliyeoa. “… Kutooa au kuoa wake wengi kunamuondolea mtu, sifa ya kazi ya askofu” (Milligan 328). Tunaweza kuwa na uhakika mara mbili kwamba asiyeoa bado, kibiblia hastahili kuchaguliwa kuwa mchungaji, kwani ndoa pia ina husishwa katika sifa katika orodha ya “ajuaye kutiisha watoto wake katika ustahivu” na “ana watoto waaminio”. “Maana inayowezekana ya kauli hii ni kwamba mtu huyo

awe na mke mmoja tu na sio mwanamke mwingine katika maisha yake” (Olbricht). Mzee ni mtu mwenye mke mmoja. Wakati anapochaguliwa kuwa mzee, awe ameoa mke mmoja.

Je, kifo cha mke wa mchungaji kinamuondolea sifa ya kuendelea kuhudumu kama askofu? Baadhi ya ndugu wanasema kwa nguvu kabisa, “Ndiyo”. Mzee anaweza kwa hiari akajiuzulu kutoka kwenye uchungaji pindi mke wake anapofariki, lakini je, Agano Jipya linamtaka ajiuzulu? Je, anakuwa amepoteza uzoefu wa maisha ya ndoa uliomwezesha mwanzo kuchaguliwa kuwa askofu?

> Swali lingine lililoibuliwa juu ya uaskofu na mahitaji ya nyumbani ni, “Askofu atafanya nini pale mke wake anapofariki? Je, ajiuzulu uaskofu Jumapili inayofuata? Wengine wanakukubali, lakini mimi sio miongoni mwao. Pale alipochaguliwa mwanzo alikuwa na mke mmoja na akafaa kwa alama ya kufanikisha kuwa na sifa. Anaweza kuamua kujiuzulu, na hiyo itakuwa ni haki yake. Hata hivyo, kwa maamuzi yangu, Maandiko hayamlazimishi kufanya hivyo. …Bado katika historia yake ana uzoefu muhimu ndani ya familia kufanikisha uzoefu wake katika ulimwengu wa utumishi ambao wazee wanautoa. …

> Chukulia mzee mwenye watoto wawili, Wakristo wazuri wenye miaka  zaidi ya 13 wenye miaka Ishirini wakafa kwa pamoja wakati wakisafiri katika gari. Jana alikuwa na watoto, leo hana, Ina maana hawezi kutumika tena? Hapana kabisa! Alikuwa na watoto, - watoto watiifu - alipochaguliwa. Alikuwa na sifa zile zote. … kwa kuwa watoto wake wamechukuliwa katika janga hili hakumuondolei sifa ya kuisimamia nyumba yake vema (Taylor 85-86).

Inawezekana kwa mgane aliyeoa tena, au mwanaume asiye na hatia aliyemwacha mkewe kwa kosa la uasherati na kuoa mwingine anafaa katika nafasi ya uzee (Mathayo 19:9; 1 Wakorintho 7:15). Kile Mungu anachokifanya kuwa si hatia kisihesabiwe juu yake kuwa ni hatia.

> Kama mke wake amekufa na ameoa tena, sheria hiyo hiyo itatumika kwenye uhusiano wake kwa mke huyu mpya. Atatakiwa awe na mke mmoja pekee. Yule aliyekufa sio mke wake tena. ***"Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai, lakini ikiwa mumewe amefariki, yu huru kuolewa na mtu yeyote amtakaye; katika Bwana tu".*** (1 Wakorintho 7: 39). Tena, ***"….bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume"*** (Warumi 7:2). Jibu la Yesu kwa Masadukayo ambao hawakuamini ufufuo linaweza pia likaonyesha kuwa baada ya kifo, muungano wa mume na mke unakuwa haupo tena (Mathayo 22:23-30). Kama mke amekufa, muungano umevunjika. Hao si mke na mume tena. Kama hili lisingekuwa hivyo, basi kuoa au kuolewa tena kusingeruhusiwa. Mume au mke hafungwi tena kwa yule mwenza aliyekufa. Kwa hiyo, akioa au kuolewa tena atakuwa na mke au mume mmoja tu. Mtu anaweza kuwa mchungaji, hata baada ya mke wake kufa ikiwa ameoa mke ambaye kimaandiko yuko huru kuolewa naye. Ni ukweli pia kwa mtu aliyetalikiana na mkewe kwa sababu za kimaandiko na akaoa mke mwingine. Atakuwa anafaa kuwa mchungaji. Hawezi kufungwa kwa mke asiye mwaminifu kwake, kama amemtaliki. (Olbricht)

Bado, kusanyiko lazima liwe na imani na wachungaji wake, na linaweza kuamua lenyewe ikiwa wanataka kumchagua mtu aliyefiwa na mke na kuoa tena, au mtu aliyemwacha mke na kuoa tena kuwa mchungaji wao.

> Kwa sababu tu mke amekufa au amekuwa si mwaminifu, mume akaamua kuoa mwingine, haimaanishi kuwa anafaa kuwa askofu. Kama hakidhi katika zile sifa nyingine, hapaswi kuhudumu. Pia kama kusanyiko halimkubali kwa sababu ameoa tena, hata kama alikuwa na haki ya kufanya hivyo, hapaswi kuchaguliwa katika nafasi hiyo ya uchungaji. Watakaopewa kazi hiyo ni wale tu wenye sifa za kimaandiko na ambao wamekubaliwa na kanisa wawe viongozi. (Olbricht)

## “Wakili wa Mungu”

(Tito 1:7)

Wakili ni meneja au mtunza hazina za mwingine, aliyeajiliwa. Wachungaji wameajiliwa na Yesu Kristo (1 Petro 5:14). Kuna mali za aina mbili ambazo wachungaji hawa wanawajibika kwa Bwana wetu; (1) Ni “mawakili wa siri za Mungu” (1 Wakorintho 4:1), na (2) Ni mawakili wa roho za kusanyiko wanalohudumia (Waebrania 13:7, 17). Eneo kubwa la uwakili ambalo wazeei wameaminiwa, linahusu mambo ya kiroho, wachungaji wanawajibika kwenye mambo ya kimwili yanayohusiana na kanisa hilo (kama vile mali na pesa). Na kwa nyongeza wanapaswa kkusimamia hata vile visivyoonekana pia (kama vile nafasi ya kuhubiri Injili). Kusanyiko hilo na vyote vinavyolihusu viko katika miliki ya mawakili wa Mungu, wachungaji.

## “Mwenye Busara”

(1 Timotheo 3:2)

“Mwenye busara” maana yake asiwe mtu wa kupitiliza. “Kila mchungaji lazima aweze kudhibiti mambo katika maisha yake mwenyewe, kama hawezi kumudu mawazo yake mwenyewe au maneno na matendo yake ya kila siku, anawezaje kutumaini kusaidia watu wengine kwa mafanikio ili wamudu kuwa sawa sawa katika kuwaza, katika kuchagua manneno na katika kuendesha shughuli za kila siku? Mtu asiye na busara hawezi kuwafanya wengine wawe na busara” (Taylor 68)

## “Mwenye Kiasi”

(1Timotheo 3:2)

“Mwenye kiasi” maana yake ni kuwa na akili timamu, aweze kujimudu, mwangalifu. Mzee anapaswa kuwa asiyependelea na anayefikiri kwa haki (Hodge 49). Hapaswi kuenenda bila uangalifu. “Mchungaji hapaswi kujiingiza kabisa katika mambo yasiyo na maana na ya kitoto. Haimaanishi kwamba hapaswi kuwa na utani au ucheshi, lakini mtu ambaye hayuko makini kwa kweli hapaswi kufikiriwa kwenye kazi hii kubwa. Kuwa mwangalizi juu ya nyumba ya Mungu ni shughuli inayohitaji umakini mkubwa” (L.R. Wilson qdt. in Taylor 69). Mzee ni mtu mwenye hekima. Anapaswa kuwa mtu mwenye akili iliyotulia, akiwa na kiasi kikubwa cha uelewa mzuri (Milligan 330).

## “Mtu wa Utaratibu”

(1 Timotheo 3:2)

“Mtu wa utaratibu” maana yake ni mtu wa kufuata utaratibu. “Maisha ya mzee yanapaswa kuongozwa vizuri. Mtu ambaye ni wa

vurugu vurugu, asiyejali na asiye na mpangilio maalum katika kazi yake hataweza kuongoza kazi ya Mungu vema. … Baadhi ya makanisa yana utaratibu katika kazi zao" (L. R. Wilson qtd in Taylor 70).

## "Mkaribishaji"

(1 Timotheo 3:2; Tito 1:8)

"Mkaribishaji, linatokana na neno ambalo kwalo tunapata upendo wa ndugu. Ukaribishaji ni upendo kwa wageni uliowekwa kwenye tendo la kutoa. Ni upendo katika kutamka ukitafsiriwa kwenye vitendo ambavyo Wakristo wanaviunganisha katika kuwatendea watu wengine. Wazee lazima wawe watu ambao nyumbani kwao ni mbingu za ukarimu. Katika eneo la ukaribishaji, mke wa mchungaji lazima ashiriki katika mapokezi ya wageni. Anashikilia funguo za mafanikio yake makubwa katika eneo hili la kifalme" (Taylor 78).

## "Ajuaye Kufundisha"

(1 Timotheo 3:2) na

### "Akilishika Lile Neno la Imani"

(Tito 1:9)

"Ajuaye **kufundisha**" na "Akilishika lile neno la imani, apate kuweza **kuwaonya** watu na kuwashinda wenye kupinga" yanatoka katia neno la Kigiriki, lenye maana ya kufundisha au kuhubiri katika mkutano wa hadhara. Moja ya sifa za kuchaguliwa kwa kazi ya wazee, inajumuisha kufundisha kwa ujasiri sheria ya Bwana mbele ya wapingaji (Tito 1:9). Kila mchungaji anatakiwa kuwa mwalimu wa neno la Mungu mwenye uwezo na mwenye nia (2 Timotheo 3:2), iwe katika faragha au hadharani. Mchungaji anapaswa kuwa na ujuzi wa kufunndisha. Jambo hili, naam, linahitaji ujuzi sahihi wa neno la

Mungu. “Mtu yeyote asiyeweza kusimama mbele ya kundi na kufundisha neno la Mungu, hana sifa za kuwa mzee au mchungaji. … Watu ambao hawawezi au ambao hawataweza kufundisha, wanashindwa katika moja ya sifa muhimu sana. … Kama mmoja hana ujuzi wa kufundisha kweli, pia hawezi kuijua wala kumpinga mtu anayepinga kweli” (Hearn, “Duties” 13).

## “Asiyezoelea Ulevi”

(1 Timotheo 3:3) au

## “Mwenye Kiasi”

(Tito 1:8)

Asiyezoelea ulevi” maana yake ni kujizuia, kutokujitumbukiza katika pombe. ”Bila ya woga wowote wa mafanikio ya ukinzani kutoka katika chanzo chochote, ninasema kwa kujiamini kabisa kwamba, mtu anayekunywa pombe hafai kwa kazi ya uchungaji wa Kanisa la Bwana. …Utumiaji wa vileo, kwa kiasi chochote, na uchungaji wa kanisa la Mungu haviendani kabisa”. Hakuna nafasi ya kunywa kistaarabu katika uchungaji.

## “Si Mpiga Watu”

(1 Timotheo 3:3; Tito 1:7) au

## “Asiwe Mgomvi”

“Si mpiga watu” na “asiwe mgomvi” yanatoka katika maneno tofauti ya Kigiriki yenye maana moja ya, asiwe mgomvi au mwenye fujo, wala asipige watu. “Kupiga (ni) … wazo la mtu anayepiga mtu yeyote na wakati wowote, kwa mtu anayethubutu kukataa au asiyempendeza; ni mtu anayeshambulia wote wanaokataa kumtumikia. … wengine wanapenda kubishana kwa jili ya vitu visivyo

na msingi" (Gugh 9). Maonyo ya kurudia-rudia ukitumia maneno tofauti lakini yanayofanana kukazia msisitizo wa Mungu hasira yanamna hii inamwondolea mtu sifa ya uzee.

## "Asiwe Mwenye Kupenda Fedha"

(1 Timotheo 3:3) Au

## "Asiwe Mpenda Mapato ya Aibu"

(Tito 1:7)

"Asiwe mwenye kupenda fedha" maana yake, hayupo kwa ajili ya pesa, asifanye pesa kama lengo lake la maisha (1 Timotheo 6:10). Yesu aliweka wazi kwamba mtu hawezi kutumikia mabwana wawili Mungu na pesa kwa uzito sawa (Mathayo 6:24). Mzee asiwe na tamaa iliyozidi ya kupata utajiri. Na wala asiruhusu hata biashara kumeza wito wake kwa ajili ya Kristo. Na hasa, mzee asifanye biashara isiyo halali (haramu) ili kutimiza tamaa yake ya fedha. Rejeo la pili kati ya sifa za mzee juu ya tabia sahihi kuhusu fedha, inaonyesha mapungufu ya binadamu na kusisitiza wema kwa wachungaji hawa wa Mungu.

## "Mpole"

(1 Timotheo 3:3)

"Mpole" maana yake ni mtu mwanana na mwenye kufikiri. Mzee lazima awe mtu ambaye muumini yeyote wa kusanyiko lake anaweza kumwendea, asiwe mkali na awe tayari kusikiliza.

## "Asiwe Mtu Aliyeongoka Karibuni"

(1 Timotheo 3:6)

Kauli hii inamaana ya Mzoefu, mwenye umri katika Ukristo, asiwe Mkristo mpya, au aliyeongoka karibuni. Mtu anayefikiriwa kuteuliwa kuwa mchungaji, sio mtu asiyehakikiwa, bali awe mwenye

rekodi iliyohakikiwa ya utumishi katika Kristo. Ni mfanyakazi mzoefu wa Bwana.

## “Ashuhudiwe Mema na Watu Walio Nje”

(1 Timotheo 3:7)

“Ushuhuda mzuri miongoni mwa watu walio nje” Maana yake hata wale wasio Wakristo wanaweza wakamshuhudia kwa wema wake. Mtu ambaye dhambi zake za nyuma bado zimefunika akili za Wakristo au wale wasio Wakristo, anakosa kuaminika kwa ndugu na hata kwa wasio Wakristo kuweza kuteuliwa kwenye jukumu hilo muhimu la uaskofu katika kanisa la Bwana. Inawezekana kwamba dhambi hizo za nyuma zimeshasamehewa na Bwana na watu pia, lakini bado *madhara* ya dhambi hiyo yanaendelea, na hivyo, kufanya isiwezekane kutumika katika maeneo fulani fulani na hasa maeneo ambayo dhambi hizo zinajulikana. “Kama kanisa halitamkubali mtu huyo, basi hawezi kuwa askofu!” (Hodge 57). “Hakuna mtu anayepaswa kuwa askofu ambaye maisha yake na tabia zake zinatiliwa mashaka, hata kama na watu wa nje.” (L. R. Wilson, *ikinukuliwa katika* Taylor 73). Kama wanajamii hawamwamini mtu huyo, anawezaje kutumika kwa ufanisi kama mzee wa Kusanyiko lenye lengo la kuwafanya Wakristo miongoni mwa hao wasio Wakristo katika jamii hiyo? Kidini, jamii inaweza kupinga ukweli wa Injili tunaoipelekea, lakini jamii inapaswa kuliamini kanisa na viongozi wake kwa uaminifu na wema wao.

Hata hivyo, ikiwa dhambi alizozifanya huko nyuma zimeshasamehewa, usidharau imani ya kusanyiko ambalo anaonekana kustahili kuchaguliwa kama mzee au ujasiri walionao jamii kuhusu heshima yake, dhambi zake za zamani, zilizosamehewa haziwezi

kumzuia mtu huyo asihesabiwe kuchaguliwa katika nafasi hiyo ya uongozi.

Mtume Paulo alikuwa muuaji, lakini aliinuka akawa kwenye utumishi wa Kikristo usiomithilika katika karne ya kwanza. Mafanikio yake mengi katika Injili ya Kristo ni katika maeneo ya ulimwengu ambayo hakuwafunga Wakristo wala kuwaua. Na pia aliandika vitabu vingi vya Agano Jipya kuliko mwandishi mwingine yeyote (Nyaraka 13). Mtume Petro alimkana Kristo, lakini alithibitisha kuwa mtumishi mwenye thamani, pamoja na mambo mengine, alihubiri hotuba ya kwanza ya Injili kwa kwa Wayahudi na Mataifa. Pia aliandika vitabu viwili vya Agano Jipya. Pamoja na kuwa Mtume, Petro pia alikuwa ni askofu (1 Petro 5:1).

## "Mwenye Kuisimamia Nyumba Yake Vema, Ajuaye Kutiisha Watoto katika Ustahivu"

(1 Timotheo 3:4) na

## "Mwenye Watoto Waaminio"

(Tito 1: 6)

"Kusimamia nyumba yake vema na kutiisha watoto katika ustahivu" Maana yake watoto wake hawashitakiwi kwa fujo, wanajiheshimu, na ni watiifu. "Kuwa na watoto waaminio" Maana yake wafuasi wa Kristo wanaoaminika, ni Wakristo.

Maandiko yanaonyesha kwamba kuwa na mtoto mmoja kunatosheleza matakwa ya Biblia ya kuwa na "watoto" (Mwanzo 21:2, 7). "Mungu anataka watoto watiifu katika nyumba ya askofu. Idadi sio kitu cha muhimu" (Hodge 53).

Vifungu hivi vinaangazia mwenendo wa watoto wa askofu wanaokaa nyumbani kwake **wakati ule tu anapochaguliwa** kuwa

askofu. Maandiko yanaorodhesha sifa za lazima mtu awe nazo **kabla** ya kufikiriwa kwenye uteuzi wa uaskofu ndani ya Kusanyiko lolote (1 Timotheo 3:1-7; Tito 1:5-9). Kifungu katika Tito kinasema *“**Ana watoto waaminio**, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi, wala wasiotii”* (Tito 1:6). Lakini, mazingira ambayo watoto hao wanatajwa, miongoni mwa sifa nyingine za wachungaji, yanaelezea iyamefunuliwa katika kifungu cha 1 Timotheo. *“Mwenye **kuisimamia nyumba yake vema**, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; (Yaani mtu asiyejua **kuisimamia nyumba yake mwenyewe**, atalitunzaje kanisa la Mungu?)”* (1 Timotheo 3:4-5).

Ni wazi kwa mujibu wa Maandiko haya kwamba ili watu wafae kuchaguliwa kama wazee (Kwa jinsi Biblia inavyosema kuhusu watoto wao), wanapaswa wawe wametunza familia zao chini ya udhibiti, akiwa na watoto Wakristo, ambao tunaweza kusema, walienenda kama Wakristo wanavyopaswa kuenenda. Wale walio katika familia yake walikuwa Wakristo waaminifu, wakionyesha Ukristo wao wazi na kwa heshima ya pale nyumbani ambapo baba yao anaongoza.

> Mwenendo wa familia ya mtu ni kithibitisho cha uwezo wake wa kusimamia masuala ya kanisa. Kama akifanya vema nyumbani kwake, basi anaweza kufanya vema hata kanisani; Lakini kama hakufanya vema nyumbani kwake, basi hatafanya vema hata kwa Wakristo kanisani. Mchungaji anapaswa kuwa na watoto watiifu. Watoto watukutu wasio na heshima, watamzuia mtu yeyote kutumika kwa mafanikio kama askofu katika kanisa. …Mtu yeyote asiyeweza kuchunga watoto wake vizuri na kwa tabia njema, sio mtu anayeweza kulichunga kanisa. (Noel Merideth, *ikinukuliwa katika* Taylor 84-85 *pamoja na ufafanuzi*).

Kisha, swali linaibuka kuhusu kuchagua mtu kwenye nafasi ya uchungaji, ambaye watoto wake wameshakua na kuondoka nyumbani. Kwa kawaida mtu anategemea mtu atimize vigezo vya askofu, ikiwa ni pamoja na watoto waaminio (Tito 1:6), wakati watoto wake hawapo nyumbani. Ni wazi kwamba tangu watoto wake walipoamini Injili, (hasa inaanzia kabla ya hili), mpaka katika kipindi kilichobaki cha miaka ya barehe wakiendelea kuishi nyumbani, mtu ambaye angeweza kuwa askofu, anajifunza (kupitia malezi) kuongoza nyumba yake. Kujifunza namna ya kuongoza nyumba yako, iliamriwa na Roho Mtakatifu kama sehemu ya kumwandaa mtu huyo kwa ajili ya uaskofu ili asaidie kuongoza familia ya Mungu pamoja na maaskofu wengine (1 Timotheo 3:1-7; Tito 1:5-9)

Fikiria kwa muda kama ingekuwa kwamba **dirisha la fursa** kwa mtu kuwa askofu linampaka wa kipindi baina ya muda wa watoto wake kuwa Wakristo na mpaka pale wanapoondoka nyumbani (labda kwenye umri wa miaka 18 au 20). Kama mtoto mkubwa alibatizwa akiwa na miaka 12, na kama wazee ama watu wengine walitegemea watoto wawili au zaidi wawe Wakristo kabla mtu huyo hajawa askofu, Je, unadhani ni miaka mingapi mtu atatumika kama mzee? Kwa mtazamo wa uhalisia, inaonyesha jambo hili lingeweza kwa kiasi kikubwa kukwaza uteuzi na pamoja na zoezi linaloendelea la uaskofu. Na zaidi si sifa zilizoonyeshwa katika maandiko wala taarifa za ziada kuhusu maaskofu, zinazoweza kupatikana kutoka kwenye kurasa zenye uvuvio, **zinafundisha** kwamba sifa za mtu kuongoza familia ya Mungu, alivyojifunza kutokana na kuongoza familia yake mwenyewe, wakati mwingine huyeyuka pale watoto wanapoondoka nyumbani. Jambo la kawaida miongoni mwa makanisa ya Kristo, linaloonyesha uelewa wa kawaida wa kifungu kinachotumika kuhusu maaskofu, **hakitafsiri** sifa za maaskofu katika namna ya kukumbatia hilo **dirisha jembamba la**

**fursa** kwa mtu kutumika kama askofu. Kwa kadiri ninavyoweza kuthibitisha kutoka katika maandiko ingekuwa hairuhusiwi, wala haina ushahidi wa kimaandiko, kuweka ukomo wa utumishi wa askofu kuwa ni miaka mitatu au minne ambayo watoto wake wanaweza kuendelea kuwapo nyumbani kwake baada ya wawili au zaidi miongoni mwao kuwa Wakristo.

Kwa upande mwingine, tabia ya watoto wakubwa wa askofu ambao hawaishi tena nyumbani kwake, sio lazima zibatilishe sifa za mtu kuwa askofu. **Maandiko yanasema hakuna kinachomgusa moja kwa moja, kama ni dhambi za watoto wake wakubwa hazimbatilishi kuendelea na uaskofu.** Akina mama na akina baba wana udhibiti mdogo juu ya watoto wao wakubwa. Mtoto mkubwa ana uhuru, na wanaweza kuamua kufanya wanavyopenda kinyume na jinsi walivyolelewa. Mara nyingi inatokea kwamba watoto wanashikilia mafundisho ya utotoni (Mithali 22:6), au kama watayaacha, hatimaye watarudi. Hata hivyo, kozi yoyote watoto wetu wakubwa wanayosomea, hatimaye inakuwa ndio wajibu wao na ndicho wanachokifanya. Maamuzi yoyote yatokanayo na tukio hilo, yawe yamefanywa na askofu au kusanyiko analotumikia, basi utakuwa ni uamuzi wa kibinadamu. Maandiko yanataka kwamba askofu lazima awe na watoto waaminio wakati wa kuchaguliwa.

Aya pekee ambayo kwayo naelewa kwamba inamtilia shaka askofu inahusiana na mashitaka dhidi ya askofu, yanayohusu dhambi katika maisha yake. ***"Usikubali mashitaka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu. Wale wadumuo kutenda dhambi, uwakemee mbele ya watu wote, ili na wenngine waogope"*** (1 Timotheo 5:19, 20). Kwa mujibu wa Maandiko, mtoto huyo mkubwa wa askofu, mmoja au zaidi, anapokosa uaminifu sio lazima amuondolee sifa asiwe askofu. Dhambi katika maisha ya askofu ni

jambo jingine. Hata hivyo, hasa, kama watoto wote wa askofu watakosa uaminifu, mtu anaweza kuhisi kwamba kuna kitu kilikosekana wakati watoto walipokuwa bado nyumbani chini ya udhibiti wa askofu na wakiwa katika kuwajibika kwake. Katika mazingira kama haya, basi, ama askofu au Kanisa analolitumikia, linaweza kuona kama ni vyema asiendelee kutumika kama askofu.

Mtu kuuongoza nyumba yake vema inajumuisha kuchukua majukumu ya mume na ubaba katika nyumba. Mtu ambaye sio kiongozi wa nyumba yake mwenyewe, hana sifa za kuwa askofu ndani ya kanisa. "Mke mtukutu, anayejitukuza anamnyima sifa mtu ambaye pengine ni mzuri. Hivyo, wake wasaidie kuwapa sifa waume zao …. Na wakati fulani watoto wanaweza kumnyima sifa baba yao" (Hearn, "Positive" 7).

## "Asiwe Mtu wa Kujipendeza Nafsi Yake"

(Tito 1:7)

Neno hili lina maana ya, asiye na majivuno. "Lazima awe mtu asiye na majadiliano katika mambo ya Imani na wajibu, lakini asiwe kichwa ngumu na asiyeshindwa katika mambo ya maamuzi na kuangalia manufaa binafsi. Diotrefe alikuwa mfano wa hayo (2 Yohana 9-11)." (Goough 9). "Mtu anayejipendeza mwenyewe yupo kwa ajili ya uongozi wa mtu mmoja tu, na mtu huyo ni yeye" (Taylor 61). Mtu anayejipendeza mwenyewe, ni toleo la mtu mzima mwenye hasira za kitoto!

## "Asiwe Mwepesi wa Hasira"

(Tito 1:7)

Neno hili maana yake ni mtu asiyechukuliwa na uchungu, asiye mateka wa hasira. "Uaskofu ni mahali pa akili zenye ukimya na utulivu,

na sio pa vichwa vya moto vyenye hasira kali na isiyotawalika. Maamuzi yanayotoka katika moto wa hasira kali hayana uwezekano mkubwa wa kuwa na busara au hekima" (Taylor 63). Watu wanaochemka au kukasirika haraka, hawana nafasi katika uaskofu Kanisani.

## "Mpenda Wema"

(Tito 1:8)

"Mpenda wema" maana yake ni mtu anayependa kilicho chema. "Hakuna kipimo kizuri cha tabia halisi ya mtu kuliko kuchunguza anachopenda na anachochukia" (Taylor 80). Eneo la upendo huu wa vitu vyema ni pamoja na kupenda watu wema (mfano, wahubiri wa Injili, walimu wa shule za Biblia, mashemasi, na wazee wenzake). Mtume Paulo aliandika sehemu nyingine kwamba, watu wanaopata raha kutoka katika mambo ya dhambi na watu wenye dhambi wanastahili kifo (Warumi 1:32).

## "Mwenye Haki"

(Tito 1:8)

"Mwenye haki" Maana yake ni kuonyesha wema wote au haki. Mzee ni mtu wa usawa asiye na upendeleo. Hana hatia ya kufanya mabaya.

## "Mtakatifu"

(Tito 1:8)

"Mtakatifu" Maana yake ni mtu wa dini aliyetakaswa. "Mtu mtakatifu ni yule ambaye ana haki mbele za Mungu" (Taylor 71).

### “Mwenye Kudhibiti Nafsi Yake”

(Tito 1:8)

Neno hili, Maana yake ni kuwa na nguvu juu ya mapenzi yake au matamanio au mahitaji yake. Mzee yuko tayari kujizuia katika dhambi au tabia mbaya. Anajinidhamisha.

## Kazi za Wazee

Wajibu wa wazee umeelezwa wazi katika Maandiko ya Agano jipya. Hakuna mzee anayehitaji kutetea ujinga kwa habari ya wajibu wake; na hakuna Mkristo anayehitaji kuwa na shaka juu ya nini wajibu wa wazee. “Wakati ambao majukumu haya ni mazito na ni mengi, yanaweza yakasomwa ndani ya Agano Jipya” (Boles, *Makanisa ya Kristo,* 24). “Wanatakiwa kufanya kazi kama waangalizi wa nyumba ya Mungu (1 Timotheo 3:5), Waangalizi, wasimamizi kwa kila eneo la kazi ya kusanyiko (Matendo 20:28), na wachungaji wa kundi (1 Petro 5: 1-3)” (Campbell 20). Wazee lazima wawe na sifa ambazo tayari zimetolewa na Mungu ili kwamba waweze kufanya kazi ya wazee mara wanapoteuliwa.

“Eneo lao la kazi haliendi mbali zaidi ya mipaka ya kusanyiko lao.” (Milligan 337). Wazee wanatumika na kuongoza makusanyiko yanayowateua kutokana na waumini wao. Rejea ya Agano Jipya juu ya wazee, inahusu Kusanyiko ambalo kwalo wametambulishwa (Matendo 20:17; Wafilipi 1:1; Yakobo 5:14). Mfumo wa kuchagua na kuteua watu ndani ya kanisa kwenye majukumu haya ni wa ngazi ya kanisa (Matendo 6:3).

Kusanyiko haliwezi kuwa juu ya viongozi wake. Ni jinsi gani wazee wenye sifa walivyo muhimu? Ukuaji wa kiroho wa kusanyiko, ukomavu na utendaji mzuri katika maeneo yote ya Ukristo yanaelemea

kwa uzito mkubwa juu ya wazee wenye sifa wanaoliongoza. Kazi za wazee zinahusu roho na zinazohusiana na hatima ya watu.

Muokaji huoka, polisi anasimamia utaratibu, mhubiri anahubiri. Hoja ni kwamba, kuna kazi ambayo imetolewa na Mungu kwa wazee kuifanya ndani ya Kusanyiko ambalo kwalo wameteuliwa. Miongoni mwa majukumu yao, wazee wanatakiwa kuwasihi na kuwaonya wanaopinga mafundisho yenye uzima (Tito 1:9). Wanatakiwa kuangalia au kuchunga roho ambazo wameaminiwa kwazo, pamoja na kuongoza (Waebrania 13:17). Kuongoza maana yake ni kuwa na mamlaka au kupewa mamlaka. Wazee hawaruhusiwi kuleta mafundisho mapya, bali wanawajibika kutumia mafundisho ya Biblia katika maisha ya Wakristo wenzao katika makusanyiko yao.

> Kanisa si demokrasia ambapo kila mtu ana sauti sawa katika kuelekeza mambo. Kanisa la Bwana linaongozwa pale mapenzi ya Mungu yanapotimizwa na mkuu wa Kanisa ambaye ni Kristo. Yeye anaongoza kupitia maaskofu. Wazee hawapaswi kuwa wakandamizaji, madikteta. Hawapaswi kuwa wakali na wasio na moyo au wasiojali, na huku wakiwatwika watu wa Mungu mambo hayo, bali wawe kama baba, wakiwa na vichwa vyenye busara na mioyo ya upendo, wanapoongoza watu wa Bwana. Mtu fulani lazima aongoze, mtu fulani lazima aelekeze kazi, mtu fulani lazima abebe nidhamu za kusanyiko. …. Roho Mtakatifu anapowafundisha wazee kuongoza juu ya kusanyiko. Kwa wakati huo huo analifundisha kusanyiko kutii oungozi wa wazee. (Boles, *Makanisa ya Kristo* 28).

## “Jituzeni Nafsi Zenu”

(Matendo 20:28)

Wazee lazima wahakikishe kwamba wanaenda sambamba na Mungu kabla ya kuongoza wengine kwa usahihi. Wazee wanajumuisha uongzi kitengo kilichoundwa ambacho kinafanya kazi sambamba mbele ya kusanyiko. Hakuna nafasi ya askofu mkuu katika uaskofu, au maaskofu wadogo au kudharauliana. Wala maaskofu wa Mungu hawawalalamikii Wakristo kwamba hawapati nafasi wakiwa na wazee wenzao. Hawakuridhishwa, wanakwenda nje na kuzunguka wazee, kwa mzee mmoja wao kukusanya waungaji mkono, ndicho hasa ambacho mtume Paulo alionya dhidi yake (Matendo 20: 29, 30). Maaskofu wa Mungu wanaenenda kwa utaratibu.

## “Litunzeni Lile Kundi Lote Nalo”

(Matendo 20:28)

Wazee lazima pia wajishughulishe na mwenendo wa kila Mkristo kanisani. Na kama ni lazima, kondoo aliyeathirika au aliyeambukizwa na dhambi, lazima aondolewe kutoka katika mizani ya kundi ili kulilinda. Wazee wakati mwingine wanawajibika kuanzisha viwango tofauti vya nidhamu ili kumwokoa mwenye dhambi na kuzilinda roho nyingine kutoka katika asili ya maambukizi ya dhambi. Wazee lazima wajue na watunze kila kondoo.

## Kulisha Kundi

(1 Petro 5: 1, 2)

Toleo jipya la King James (Biblia ya Kiingereza), linatumia neno “Kuchunga kundi” mahali pa Kulisha kundi la Mungu katika toleo la Biblia ya King James. Sehemu kubwa ya kile anachofanya mchungaji

kuhusu kondoo wake ni kuwalisha. Wazee wanahitajika kutoa chakula cha kiroho kwa kundi hili la Mungu. Wazee wataliongoza mbali kutoka kwenye chakula cha kiroho chenye sumu, na kuwapeleka kwenye chakula cha kiroho chenye afya kitakachosaidia kondoo kukomaa.

Wazee watalilisha na kufundisha kanisa (Matendo 20:28). Wazee wanaweza kutumia mali zilizopo kuwasaidia kutimiza majukumu yao. Rasilimali watu inajumuisha; Mashemasi, Walimu, Wahubiri, na Wamisionari. “Sio kosa kwa wazee kuuliza au kuomba ushauri kutoka kwa wengine ndani ya kusanyiko, ambao wanaonekana kuwa na hekima au wajuzi kuliko wao. Wazo lolote lenye akili lililoletwa na wengine, linapaswa kuzingatiwa kwa umuhimu unaostahili.” (Hearn, “Duties” 14).

## Kusimamia Kundi

(1 Petro 5:2)

Wazee wanao wajibu wa kulisimamia kundi ili kuwapa mahitaji yao kwa njia ya kumchunga mtu mmoja mmoja. Wanalazimika pia kujaribu kurejesha sehemu salama wale wanaopotea. Kusimamia kundi ni namna nyingine ya kuhamasisha haja ya wazee kuwa ni mawakili wa Mungu kwa watu wake. Kusimamia kunakuwa kuzuri ikiwa wale wanaosimamiwa wanawatii wale wasimamizi.

## Kuwa Kielelezo

(1 Petro 5: 3)

Wazee wanajitoa wenyewe kuwa kama kielelezo cha ndugu kufuata. Kama wazee wako vile ambavyo Mungu anawataka wawe, mfano wao utawasaidia ndugu katika Kristo kuepuka dhambi katika maisha yao (1 Wakorintho 11:1). Wazee wanatakiwa kuwa kielelezo, lakini wanatakiwa kuwa zaidi ya kielelezo. Wanatakiwa kuwa

wachungaji au kusimamia makundi yao husika (1 Petro 5:2), lakini bila ukali au udikteta (1 Petro 5:3). "Kinachokatazwa katika somo hili linaloendelea ni matumizi mabaya ya mamlaka, na sio matumizi yake mazuri" (Woods 30). Wazee wanatakiwa kutumika kama kielelezo kinachofaa kufuatwa na wengine kanisani, mara zote wakizingatia kwamba wanawajibika kwa "Mchungaji Mkuu", Yesu Kristo (1 Petro 5:4).

## Kuwa Makini na Mbwa-mwitu

(Matendo 20: 29, 30)

Wazee lazima wawe makini na walimu wa uongo ambao wataliongoza kundi wanalolichunga mbali na mafundisho ya uzima (Warumi 16:17, 18; 2 Timotheo 4:3). Hatari inaweza kutoka nje ya kanisa ama hata ndani ya kanisa. Mtume Paulo aliwaambia wazee kutoka Efeso kwamba walimu wa uongo wanaweza kuinuka kutoka miongoni mwao (Matendo 20:29). Wazee walio macho wanachambua kile mhubiri na mwalimu wanchofundisha na kuhubiri kuhakikisha ndugu hawakudhurika na mafundisho ya uongo. Inapogundulika mafundisho dhaifu au ya kurudisha kundi nyuma, wazee wanaweza kufanya lolote ili kuzuia madhara. Kadiri muda unavyokwenda wazee wanatakiwa kuyaona madarasa yanavyofundishwa ili wajue.

## Kuziba Vinywa Vyenye Maneno Yasiyo na Maana na Wadanganyaji

(Tito 1:10, 11)

Wazee wanatakiwa kutambua walimu wa uongo waliojificha kwenye ualimu na uhubiri wa Injili kabla roho hizi zenye thamani hazijadhurika na mafundisho ya uongo. Wazee wanahitaji hamasa ili kupinga mabadiliko ya kimakosa miongoni mwa watu wa Mungu

ambao wanawachunga, na makosa hayo yanaweza kuonekana waziwazi au kwa kificho. Kila mhubiri wa Injili na mwalimu wa Biblia anapaswa kujua kwamba ikiwa ni lazima basi wachungaji wake watasimama wakati anapoongea na kanisa ili kumsimamisha au kusahihisha mafundisho yake (Yakobo 3:1).

## Kuwasaidia Wanyonge

(Matendo 20:35)

Katika kila kanisa kuna Wakristo wachanga ambao hawawezi kujilinda wenyewe kikamilifu. Wazee lazima wawakinge na kuwahamasisha Wakristo hawa wanyonge. Wazee lazima wapange na kutoa mpango wa kuwalisha mpaka wafikie hatua ya ukomavu. (Waebrania 5: 12-14).

## Kuwaombea Wagonjwa na Kushughulikia Mahitaji Yao

(Yakobo 5: 16)

Kila Mkristo anao wajibu juu ya Mkristo mwenzake, na Mkristo yeyote anapaswa kuwaombea wagonjwa, na kuwafanyia kile kinachotakiwa kama inawezekana. Hata hivyo, wazee hawawezi kuepuka wajibu wao mkuu wa kuwaombea wagonjwa na kushughulikia mahitaji yao kwa kuwatumia wengine kama vile mhubiri. Wazee hawawezi kuwapa watu wengine kazi zao.

## Kujadili na Kuamua Mambo ya Kanisa

(Matendo 15: 6)

Lazima kuwe na watu ambao wataamua mambo ya kanisa. Hii ni kwa mambo ya kimwili na pia ya kiroho kuhusu kanisa hilo. Mungu

amepanga kwamba wazee wabebe jukumu hilo. Wazee wanajizoeza wenyewe katika eneo lenye kufaa au lenye manufaa.

## Kuchagua na Kusimika Walimu na Wahubiri

(1 Timotheo 4:14)

Timotheo alichaguliwa na kusimikwa na wazee. Kwa kawaida wazee ndio wanaochagua wahubiri wa Injili na wanawajibika pia kwa kila mwalimu ndani ya kanisa ambalo kwalo wamesimikwa.

## Kukesha kwa Ajili ya Roho za Watu

(Waebrania 13:17)

Hakuna kitu kilicho cha muhimu kuliko kuwajibika kwa Mungu kwa ajili ya roho za wengine. Wazee wanabeba mzigo huu mkubwa. Mzigo huu ungekuwa mwepesi kama washirika wengi wangeshirikiana na wazee wao kwa vile wanavyojaribu kuwaelekeza kwenye fukwe za milele za Mbinguni. Wazee lazima wakeshe kwa ajili ya roho za watu kwa namna ile ile ya Ezekieli 33:7-16 walivyowajibika kuwaonya wenye dhambi kwa dhambi zao. Wazee ni wachungaji wa roho ambazo ziko katika uangalizi wao.

Wazee ni lazima wajishughulishe kumpa kila Mkristo mahitaji ya kiroho. Wao ni mawakili wa roho zilizo katika uangalizi wao, huku wakiongoza makusanyiko yao kwa niaba ya Bwana wetu. “Mchungaji wa kweli atawajua kondoo wake wote, ni akina nani, wako wangapi, wanaishi wapi, na hali zao kiroho zikoje” (Hearn, “Majukumu” 13).

## Kuchagua na Kusimika Wazee

Wazee hawajiteui wala kujichagua wenyewe (Matendo 14:23; Tito 1:5). Watu wanaokuwa wajibu huu wenye umakini na kuchaguliwa

na Wakristo wenzao kwa mujibu wa sifa za Mungu. Halafu Roho Mtakatifu anawasimika (Matendo 20:28) katika uongozi (Kama kweli wana vigezo) ***wakati ule kanisa linapowachagua***. Hata hivyo, wazee wametengenezwa na sio kwamba wamezaliwa hivyo, na wanaweza kuharibiwa pia (1 Timotheo 5:19, 20).

“Usifanye makosa juu ya hili, suala la uchungaji ni shughuli nyeti. Haipo kwa ajili ya vijana wadogo, wala haipo kwa wale wasio viongozi, na haipo kwa wale ambao vipaumbele vyao ni fedha ila kwa ajili ya Bwana, na kwa uhakika si kwa ajili ya wenye mioyo ya kukata tamaa” (Campbell 20). Chagua na simika wazee kwa uangalifu, kwa sababu ni rahisi kuweka watu sahihi kwenye nafasi hiyo kuliko ilivyo kuwaondoa wazee wasio na sifa. Kanisa la Bwana ni la muhimu sana na lina gharama sana (Matendo 20:28) kuweza kuliweka kwenye hatari ya kuharibika kwa kusimika watu wasio na sifa kuwa wazee.

“Ufunguo wa kuwa na wazee bora uko katika kuchagua watu wenye sifa” (Hodge 45). Kuchagua na kusimika wazee kusishushwe hadhi na kuangalia suala la umaarufu. Wazee wasichaguliwe wala kusimikwa kutegemea ushindi wa kisiasa au mafanikio kibiashara. Wazee wasichaguliwe kwa sababu ya mahusiano ya kifamilia na watu wengine iwe ndani au nje ya kanisa. Kuwa na sifa za kielimu au kutokuwa pekee yake haipaswi kuwa kigezo cha mtu kuteuliwa kuwa mzee. Utajiri binafsi wa mtu hauwezi kuwa sababu ambayo kwayo atachaguliwa kuwa mzee. Kwa kweli mtu ambaye anawakandamiza wengine na jeuri kwa wenzake hafai kuwa mchungaji wa Bwana. Makanisa ya Kristo yatajiweka yenyewe kwenye anguko baya kama umakini wao kwenye sifa za wazee utazunguka kwanza kwenye maswali haya mawili; (1)“Je, ndoa yake kibiblia ni sahihi? Na (2)Je, ana watoto waaminio?” Kuwa mzee wa Mungu, sifa mbali mbali za kiroho zinazopatikana katika Biblia zinahitaji kuzingatiwa pia. Kanisa lisitulie tu

kwa wale “**bora waliopo**” (Hodge 46) huku likiacha zile sifa muhimu za kibiblia za wazee. “***Hakuna watu wakamilifu kabisa***! Sifa zote zilizoorodheshwa lazima ziwepo katika kila mzee kwa kiwango kinachokubalika. Lakini ***nguvu ya wazee iko katika wingi wao***. Kile ambacho mmoja hana mwingine anacho” (Hodge 47)

Habari za kutosha zinapatikana katika Agano jipya, kuonyesha wazi kabisa kwamba kila kusanyiko linapaswa kuwa na wingi wa wazee (Matendo 14:23; 20:17; Tito 1:5). Hata hivyo, ni wazi kwamba kabla ya kuteuliwa maaskofu katika kusanyiko lolote lililo hai, litaendeshwa kwa kipindi cha mpito na uongozi unaokubalika bila ya kuwa na wazee. Zaidi sana sifa za wazee zinapatikana katika (1 Timotheo 3:1-7; Tito 1:6-11; Waebrania 13:17) na majina yanayotumika kuwataja (Wachungaji, Waefeso 4:11; Waangalizi, Matendo 20:28; Wazee, 1 Petro 5:1-4) yanaonyesha kazi zao. Hata hivyo, karibu kila kitu kingine kinachohusu wazee kimeachwa na Mungu katika ulimwengu wa manufaa. **Hatuna taarifa yoyote kibiblia kuhusu utaratibu wa kuchagua na kusimika wazee.** Taratibu hizi hazikuwekwa na hivyo, sio suala la Maandiko. Na kwa hiyo sio suala linalotoa mshituko wala kutokuelewana.

> Hakuna njia iliyowekwa wazi katika Agano Jipya kwa ajili ya kuchagua na kusimika wazee. ….. Hakuna maelekezo yaliyotolewa yanayotufundisha jinsi walivyoteuliwa au jinsi ambavyo wangekuwa wanateuliwa. Kwa kuwa hakuna Maandiko yanayotufundisha jinsi walivyokuwa wanateuliwa, tumeachwa huru kuwateua kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ambayo haipingani na taratibu za Maandiko, na wakati huo huo zinazo hamasisha kuungana kwa Wakristo. (Boles, *Makanisa ya Kristo* 15)

> Kwa kuwa hakuna njia moja ya kuweka wazee iliyowekwa wazi katika Biblia, mifano ya kuchagua wahudumu katika (Matendo 6) inaweza kuwa ni njia nzuri ya kufuata. Mtume alilishauri kanisa kuangalia miongoni mwao watu wema watakaotumika katika nafasi hii. Hivyo tu, kanisa, baada ya kufundishwa na kuelekezwa katika mambo haya muhimu, linaweza kuchagua wanaume ili watumike kama wazee. Njia haijaelezwa katika Maandiko. (Hearn, "Uchaguzi" 5).

Pasipo wazee, Wakristo wanaume wa kusanyiko husika wanawajibika kwa mambo ya kanisa mpaka wakati ambao kanisa litakuwa na wazee. Kanisa lina wajibu wa kuchagua  wanaume wenye sifa kutumika kama wazee. Si sahihi kibiblia kwa kanisa kutokuwa na wazee kwa muda mrefu, kama wanaume wenye sifa wapo katika kanisa husika. Na pia itakuwa kinyume cha Biblia kwa kusanyiko kuweka namna ya uongozi, unaoitwa kamati (au mtu mmoja n.k), badala ya kufuata maelekezo ya Biblia ya kuweka wazee (labda iwe hakuna wanaume wenye sifa watakaotumika kama wazee, kwa maana ya washirika wanaume wa kusanyiko).

Na sio nadharia ya vitendo ya kawaida, bali ni uongozi wenye hekima wa wazee ambao utachangia kudumu kwao madarakani. Iwe inapaswa kuwa na nyongeza ya wazee wengine kuwekwa kabla ya kujiuzulu kwa mzee au kushindwa kunakotarajiwa au kifo cha mzee pale ambapo uongozi unaonekana kudhoofika inabaki kuwa ni suala la maoni na faida. Pengine wazee wanaweza kuwaweka mbele ya kanisa wanaume ambao wanawapendekeza wawekwe katika uongozi. Kwa hakika, Ingawa mwaka baada ya mwaka, wachungaji wa kanisa husika la Mungu, watawatayarisha wanaume na wanawake kiroho kwa ajili ya

utumishi mkubwa. Tunategemea kupata wazee watarajiwa pamoja na wake zao miongoni mwa hao wanaoandaliwa kwa utumishi. Kufundishana (2 Timotheo 2:2) mafundisho ya Kristo (Waebrania 6:1; 2 Yohana 9) pekee kutafanya kuwe na muendelezo wa kuwatayarisha Wakristo waliojitoa kujaza nafasi ya wazee wakisindikizwa na wake zao. Hata hivyo, kusanyiko linaweza likawa halina wazee bado. Au l inaweza kuwa kwamba uongozi wa kanisa umejiuzulu (labda kwa sababu ya kifo cha mzee mmoja au wawili). Je, kanisa litachaguaje wazee wakati ambapo hakuna wazee wakati huo?

Ikiwa ni maoni ya uongozi uliopo au uliochaguliwa na washirika wa kanisa, wanaume Wakristo lazima wachunguzwe kabla ya kuteuliwa kuwa wazee. Mara nyingi mhubiri, mzee au walimu ndio wanaopitia wakiwa pamoja na kanisa kwa wiki kadhaa, sifa za wazee kibiblia. Tunatumaini baada ya kupitia huku wakiheshimu sifa anazotaka Mungu kwa wazee, kanisa litakuwa limejiandaa vyema kuchagua na kusimika wazee sawa sawa na neno la Mungu.

Kwa kawaida katika siku hizi, majina ya wanaume Wakristo, yanatajwa mbele ya kanisa ili wakaguliwe. Watu wowote ambao majina yao yamewekwa mbele, lakini hawatamani kutumika kama wazee, wanaweza kujitoa wenyewe katika kufikiriwa. Mara kwa mara kwa wiki mbili zinazofuata ndugu wanashawishiwa kuweka wazi jambo lolote linalohusu uteuzi, na wasiwasi huo utachunguzwa. Wakati mwingine ndugu wanajitoa wenyewe kwa hiari, wakati huu, kutoka kwenye uwezekano wa kuchaguliwa kuwa wazee. Vinginevyo kama wasiwasi kuhusu uteuzi umetatuliwa kikamilifu kwa watu au kwa wazee, basi ndugu hao na wengine ambao kwao hakuna aliyeonyesha mashaka, watatambuliwa kama wazee wa kanisa hilo tangu siku hiyo. Wahitaji wengine kwa ajili ya uteuzi wa uaskofu, wanaume ambao

kwao, wanaume wa kanisa au maaskofu hawawezi kutatua malalamiko kuhusu wao kikamilifu, hawawezi kutambuliwa kama wazee.

Njia yoyote ambayo imekubbaliwa na kanisa husika inafaa kwa uchaguzi na uwekaji wazee ilimradi tu isivunje misingi na mafundisho ya Biblia. Hata hivyo, lazima wachaguliwe sawa sawa na zile sifa zilizotolewa katika Biblia za wazee. Na bado sherehe au shughuli rasmi kuendana na utamaduni wa kusanyiko, lazima viende mbali katika (1)Kukuza hali ya kutambua upekee na umuhimu wa kuchagua wazee (2)Kurasmisha uchaguzi wa wazee kwa ndugu wote na makanisa jirani pia. Kwa hali yoyote kanisa hilo linawajibika kuchagua na kusimika wazee wake lenyewe. Tuna mfano katika Maandiko ya Agano Jipya wa kanisa kuchagua wanaume kwa kazi maalum ndani ya kanisa (Matendo 6:3). Katika Matendo 6:1-6, kanisa lilipewa maelekezo kuhusu sifa za watu watakaochaguliwa. Kanisa lilielekezwa kuchagua wanaume miongoni mwao kwa kuzingatia sifa zilizoelezwa. Kwa kawaida kama kusanyiko halijaridhishwa na viongozi wake, halitawafuata. Kanisa linatakiwa kuchagua viongozi wake lenyewe. Halafu mitume waliwasimika watu ambao walikuwa wamechaguliwa na kanisa. Tena tuna mfano mwingine wa kibiblia wa kuchagua kwa dhati kabisa watu kutoka ndani ya kanisa kwa kazi maalum (Matendo 13: 2, 3).

## Hitimisho

Ni wazi, Mungu aliweka sifa za wazee katika Agano Jipya kwa sababu aliwaona kuwa ni muhimu na wa lazima na sio hiari. Kwa hiyo, Wakristo lazima tujue kile ambacho Agano Jipya linafundisha kuhusu wazee. Wazee, maaskofu, waangalizi, wachungaji ni visawe au maneno yanayotumika kwa kubadilishana yanayotoka kwenye Kigiriki; *presbutero, episkopos* na *poiman.* (Matendo 20:17; Tito 1:5, 7). Wingi wa wazee daima wanatumika pamoja juu ya kanisa lililo na muundo

kamili (Matendo 14:23; 20: 17; Wafilipi 1:1; 1Timotheo 5:17; Tito 1:5; Waebrania 13:17). Hivyo, hii ina maana kuwa kila mzee ana mamlaka sawa na mzee mwingine katika kanisa hilo, hakuna askofu mkuu, wala maaskofu wadogo. “Watu hawa wako sawa kimamlaka, na wana kauli sawa katika majukumu yao yote kama wachungaji wa kundi” (Bryant 11).

Hakuna ofisi yenye wajibu na utumishi iliyo kuu kuliko hii ya wazee. Wana majukumu yaliyo muhimu sana hapa duniani! **Moja ya sifa zinazolielezea kanisa ambalo Yesu alilifia na ambalo kwalo yeye ni kichwa ni kanisa lile lenye muundo kamili, likiwa na wazee wenye sifa za kibiblia.**

Wakristo wanayo haki ya kutarajia kwamba **kila** mwanaume anayetumika kama mzee, awe na **kila** moja ya sifa za kibiblia za wazee (1 Timotheo 3:1-13; Tito 1:5-9). Tunayo haki ya kuwatarajia wazee kuongoza na kulisha kundi ambalo wamechaguliwa juu yake (Waebrania 13:17; Matendo 20:28; 1 Petro 5:2). Pale tu ambapo wazee wenye sifa kamili wanapotumika katika kila kanisa, makanisa ya Kristo yatafanya kazi kwa ushirikiano na kwa mapenzi ya Mungu. Mungu alijua alichokuwa anakifanya pale alipoamua kwamba kila kanisa liongozwe na ***wingi wa wazee*** wenye sifa za Kimaandiko.

# Uongozi wa Kiume katika Nyumba

## Hapo Mwanzo

Uhusino wa wajibu wa mwanaume na wajibu wa mwanamke (yaani mwanamke kuwa chini ya mwanaume) unahusiana na asili ya kila jinsia, na wajibu wa mwanamke kumsaidia mwanaume tokea wakati wa uumbaji. ***"Maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume. Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume"*** (1 Wakorintho 11:8, 9). Zaidi sana, mpangilio wa uumbaji umeathiri wajibu husika wa mwanaume na mwanamke. ***"Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza na Hawa baadaye"*** (1Tomotheo 2:13). Na zaidi tena, mwanamke akiwakilishwa na Hawa, alikuwa mwanadamu wa kwanza kufanya dhambi ***"Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa, akaingia katika hali ya kukosa"*** (1 Timotheo 2: 14). (Adamu alitenda dhambi kwa kule kujitoa kwake kwa Hawa, na kushindwa kwake kuongoza kama Mungu alivyokusudia. Maandiko, kwa asili, hayamsafishi Adamu katika dhambi yake).

Wanawake kuwa chini ya wanaume ni sheria iliyotolewa na Mungu ambayo imekuwepo kabla ya Ukristo na kabla ya dini ya Kiyahudi. Mungu alianzisha wajibu husika kwa mwanamke na mwanaume katika Bustani ya Edeni mwanzoni kabisa mwa kipindi cha mababu. *"Akamwambia mwanamke hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako, kwa utungu utazaa watoto,* ***na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala****"* (Mwanzo 3:16). Kwa hiyo, wajibu wa mwanamke kuwa chini ya mwanamume hauna uhusiano na mila wala tamaduni, bali umekuwepo kabla ya hivyo vyote. Na pia, Injili

haikubadilisha wala kuondoa wajibu wa mwanamke kuwa chini ya mwannaume kama ambavyo haikuathiri pia; (1) Kuzaa kwa uchungu (2) Kula kwa jasho (3) Kifo cha kimwili (Mwanzo 3:1619), ambavyo kwa pamoja vitabaki mpaka mwisho wa nyakati.

## Kipindi Chote Cha Mababa na Cha Torati

Kipindi cha mababa ni kipindi tunachokiita, kati ya uumbaji wa Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni mpaka kuanzishwa dini ya Kiyahudi wakati zilipotolewa Amri kumi na Mungu kwa Waisraeli. Neno mababa (Patriarchy) ni neno jumuishi lenye maneno mawili; "Baba" na "Uongozi." Mungu aliongoza kupitia mababa wa familia. Mungu aliwasiliana na baadhi ya mababa, waliokuwa wanawajibika kueneza neno lake kwa familia zao na nyingine pia.

Baadhi ya mababa ambao Mungu aliwasiliana nao nyakati hizo ni wahusika wakuu katika Biblia; Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Kwa habari ya yale mawasiliano toka kwa Mungu, Mume, ambaye pia ni baba wa familia, alipewa majukumu ya kuongoza familia yake. Kwa Ibrahimu, Mungu alisema, ***"Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana, wafanye haki na hukumu, ili kwamba Bwana naye akamtimizie Ibrahimu ahadi zake"*** (Mwanzo 18:19). Kwa uvuvio mtume Petro aliona kwamba Sarah alimtii Ibrahimu. *"Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao. Kama vile* ***Sara alivyomtii Ibrahimu,*** *akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yo yote"* (1 Petro 3:5-6).

Pia chini ya dini ya Kiyahudi, uongozi wa wanaume majumbani uliendelea kama ulivyoanza katika Bustani ya Edeni. Matokeo yake, Hesabu 1:4 inaongelea ***"Kichwa cha nyumba ya baba zake."*** Zakaria

alithibitisha jina lililotolewa na Elizabeth la mtoto wao Yohana, kitendo kilichomaanisha kwamba, kama mume na baba, Elizabeth aliwajibika kumtii (Luka 1:59-63). Msingi wa Agano la Kale ambapo unapoangalia familia za Kiyahudi unaonyesha uongozi wa wanaume majumbani uliendelea kipindi chote cha dini ya Kiyahudi.

## Katika Ukristo Pia

Sababu zinazotolewa na maneno matakatifu ya Mungu kwa wajibu husika wa mwanaume na mwanamke zimekuwepo kabla ya hizi kuwepo, yaani, hizi tamaduni zetu. Kwa hiyo, uzingatiaji wa tamaduni zetu hizi haustahili kwa haya majukuu yaliyotolewa na Mungu kwa wanaume na wanawake. Agano Jipya kwa uwazi kabisa linatoa majukumu yaliyo tofauti kwa wanaume na wanawake. Hakuna kitu katika Maandiko au hata ambacho kwa namna yoyote kitapunguza au kuchepusha, au kubadilisha kile ambacho Mungu amesababisha kiandikwe kwenye kurasa zilizovuviwa kuhusu somo hili.

1 Wakorintho 11 iliandikwa ili kuanzisha upya miongoni mwa "Wakristo Wakorinto" uhusiano wa majukumu ya wanaume na wanawake na kila mmoja akiwa chini ya Ukristo. ***"Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu"*** (1 Wakorintho 11:3). Ukweli huu unatumika kote katika Kanisa la Bwana na hata nyumbani. Inajirudia katika Agano jipya ambapo utakuta wanaume wakitawala majumbani. ***"Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu, kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa, naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo"*** (Waefeso 5:22-24). ***"Kadhalika ninyi wake watiini waume zenu, kusudi ikiwa wapo***

***wasioamini Neno, wavutiwe kwa mwenendo wa wake zao pasipo lile Neno"*** (1 Petro 3:1).

Kibiblia wajibu wa wanawake kuwatii wanaume katika nyumba na katika kanisa hauwapi wanaume haki ya kuwanyanyasa wake zao. ***"Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake;"*** *(Waefeso 5:25).* ***"Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe"*** (Waefeso 5:28).

Majukumu tofauti ya mwanamume na mwanamke yanabaki vilevile. Licha ya **masahihisho ya Kisiasa** katika jamii za kisasa. Labda hakuna kitu kizuri kinachoweza kuelezea wajibu usiobadilika wa mwanamume na mwanamke kama Mungu alivyotaka uwe kuliko ukweli usiobadilika kwamba wanawake wa vizazi vyetu lazima wazae watoto. Mtume Paulo alitaja kuhusu wajibu huu katika 1 Timotheo 2:15, ***"Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso pamoja na moyo wa kiasi."*** Mwanamke haokolewi kwa uzazi lakini hoja ya kifungu hiki ni kwamba hawezi kutarajia kukubaliwa na Mungu ikiwa atatelekeza wajibu ambao Mungu amempa mwanamke.

Kuna usawa wa kiiblia kati ya wanaume na wanawake kuhusiana na wokovu kama inavyoonyeshwa katika aya zifuatazo, ***"Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu"*** (Wagaatia 3:26-28). Hata hivyo, majukumu kati yawanaume na wanawake ni tofauti.

# Uongozi wa Kiume Kuhusiana na Familia ya Mtu

Hisia kutoka katika 1 Timotheo 5:8, ni kwamba kimsingi kichwa cha nyumba (familia) ana wajibu wa kuhudumia familia yake – ikiwa ni pamoja na ndugu wengine ambao miongoni mwao huenda kuna wajane kulingana na muktadha huo. ***"Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini."*** Kuna njia mbili za msingi ambazo uongozi wa mwanamume unajidhihirisha wenyewe; Uongozi wa mwanamume kwa mke wake na uongozi wa mwanamume kwa watoto wake.

# Uongozi wa Mwanamume kwa Mke Wake

Sio tu kwamba Sara alimtii na kumheshimu Ibrahimu chini ya kipindi cha mababa, mtume Petro alitumia ukweli huo kama mfano kwa wanawake kuwatii waume zao kipindi hiki cha Ukristo. (1 Petro 3:5-6). Haitoshi kwamba wake kwa hiari wanawatii waume zao, lakini waume wanahitajikakukumbatia majukumu yao ya nyumbani waliyopewa na Mungu. Kama waume na mababa hawayakubali majukumu yao hapo nyumbani, huo uwazi hautaendelea, bali wake na watoto watayapokea. Lazima mtu achukue madaraka ya nyumbani, na kufanya maamuzi. Kama mume hachukui madaraka, mke wake atayachukua – kama sio kwa sababu nyingine, kwa sababu tu, lazima mtu fulani ayachukue.

Mafundisho katika Maandiko kwamba mke lazima amtii mume wake, yanaweka majukumu ya nyumbani kwa mume. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni kwa kiasi kikubwa, kwa sababu ya mabadiliko ya kijamii, majukumu ya kisasa ya wanaume na wanawake

yameboreshwa na kuwa mbali na vile Mungu alivyotaka. Maandiko, ingawa hayajabadilika, wala hapajawa na ufunuo wowote kwa karibu zaidi ya miaka 2,000. Kwa kadiri Mungu na wana wa Mungu wanavyohusika, wajibu husika kwa wanaume na wanawake uliotolewa na Mungu hauathiriwi na mambo ya kisasa. Jitihada za kutumia **masahihisho ya kisiasa** kwenye majukumu ya kibiblia yamepotoshwa.

Mke wangu kwa moyo mweupe alichunguza kwa malengo, kama hisia zinazowezekana, alizoanza kuziona akiwa anafanya kazi nje ya nyumbani. Kama mwanamke Mkristo amehitimu kabisa kuweza kufupisha baadhi ya hatari kwenye mipangilio ya Mungu ya nyumbani pale wanawake wanapoenda kufanya kazi nje. Wakati huo huo mwanamke Mkristo anaweza kutofautisha hatari hizo na mapenzi yaliyofunuliwa na Mungu kuhusiana na majukumu ya mwanamume na mwanamke. Bonnie aliandika:

> Wanachofanya wanawake wengi wanaofanya kazi nje ya nyumbani katika miaka ya karibuni inachangia kuchanganya "wajibu wa wanawake" … Kadiri muda unavyozidi ambao wanautumia huko nje wakipata vipato vyao wenyewe vinavyolingana na hata kuzidi vile vya waume zao ndivyo wanawake wengi wanavyofurahia kuwa mbali na nyumbani na mbali na familia zao … Wakiwa na kazi za "*kufanya maamuzi*" huko kazini kwao, wanawake wanaanza kuamini wanaweza kufanya maamuzi hata nyumbani kwao na kuwa na kauli ya mwisho pia. Kupata kipato ambacho ni chao pekee kumefanya iwe rahisi kupata talaka kuliko kutatua matatizo pale majukumu yaliyotolewa na Mungu ya mkuu wa nyumba yanapoanza kuvunjika. Bahati mbaya, watoto ndio wanaoathirika, na

kadiri muda unavyoendelea watoto wanayarudia madhaifu ya wazazi wao. Unaanzishwa mduara ambao sio rahisi kuuvunja.

Kama mke, mwanamke ni zaidi ya mwenza. Ni mshirika wa mume katika utafutaji wa malengo ya kidunia na hata ya mbinguni kupitia majukumu tofauti. Mwanamke mtiifu na mwajibikaji anastahili upendo na kutendewa mema na mume wake (Waefeso 5:25, 28, 33; Wakolosai 3:19; 1 Petro 3:7). Aquila na Prisila ni mfano mzuri ndani ya Biblia wa ushirikiano wa mume na mke unaostahili kuigwa. 1 Petro 3:7 inasoma, ***"Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe."*** Wajibu wa mume unafanikisha wajibu wa mke wake wa utii pindi anapomhudumia na kumsifia. Wao ni washirika, na mume ni kiongozi wa ushirika huo.

Kiukweli Mungu amewapa wanawake kazi za kufanya; (1) Ambazo inabidi wazikubali ili kumfurahisha, (2) majukumu ambayo yanapaswa kupokewa kwa furaha, na (3) ambayo kwayo wanawake wanastahili pongezi kwa kazi nzuri. Uongozi wa wanaume majumbani kuhusu mke wake unajumuisha kuonyesha upendo kwao na kuwapongeza kwa yote wanayoyafanya ili kupafanya nyumbani pafae. Uongozi wa wanaume unamheshimu mama watoto wake kwa kumuwezesha kumudu majukumu ya nyumbani, ikiwa ni pamoja na watoto wao. Mume na baba ni nusu tu ya ushirikiano huo, pamoja na mke wake na mama watoto wake, akiwa ni upande mwingine wa ushirikiano, inayoongoza pale nyumbani. Mwanamke Mkristo atautii uongozi wa mume Mkristo, lakini ni rahisi kwake kutii kwa mwenza mzuri anayeyabeba majukumu ya kuongoza pale nyumbani.

> Tunapogundua kuna hitaji la kitu fulani kufanyika, hatuangalii picha ya jumla. Hivyo, tunaingia ndani na kufanya kile kinachotakiwa kufanyika, bila kugundua kwamba tunaweza kuwa tunakanyaga sehemu ya Mungu kwa ajili yetu katika nyumba zetu na katika kanisa. Naamini kwamba kama watu wangegundua kwamba Mungu ana mpango na majukumu kwa ajili yao na kama wangeyapokea kwa utayari na kuyafanyia kazi, wanawake wasingefikiri kwamba wanahitaji kuingilia na kuwasaidia wanaume katika majukumu yao …Wanaume wanaposhindwa kupokea na kufanya wajibu wao, kama waume na akina baba, wanawake wanahisi "kwamba kama kitafanyika, inabidi nikifanye." (Bonnie Rushmore)

Ni kosa la mwanaume mwanamke anapochukua majukumu ambayo Mungu hakumpatia katika nyumba. Ni makosa yake kwa sababu anamruhusu (mwanamke) kuacha majukumu yake na kuteka majukumu ya mwanaume. Mara kwa mara wanakosea kwa kuacha bila kufanya yale ambayo wangepaswa kuyafanya kwa makusudi au kwa bahati mbaya, kwa kumwachia mke wake ayafanye. Nyumba itakuwa na mpangilio mzuri pindi kila mmoja anapotimiza majukumu yake.

## Uongozi wa Kiume Kuhusiana na Watoto Wake

***"Ninyi akina baba msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana"*** (Waefeso 6:4). Akina mama (na akina bibi pia) wanatimiza jukumu muhimu katika kuwalea watoto (2 Timotheo 1:5). Katika nyumba, mke ambaye ni mama kwa kiasi kikubwa ana majukumu ya nyumbani (1 Timotheo 5:14; Tito 2:1-5).

Eneo hili la huduma ya kimungu inamjumuisha mama katika uangalizi na uongozi wa watoto wadogo. Mama hana jukumu muhimu zaidi mbele ya Mungu kama kuongoza vizuri familia yake. Licha ya hayo, Mungu anamuona baba ndiye mwenye wajibu wa mwisho wa kulea watoto. ***"Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa"*** (Wakolosai 3:21).

Kama baba haitumii ile mamlaka iliyowekwa na Mungu ndani yake kwa mujibu wa Maandiko, basi watoto watajiongoza wenyewe. Kama ni lazima sana, watoto huwa wanajilea wenyewe, na hili sio jambo zuri sana. Na wala Mungu hakukusudia akina mama kulea watoto pasipo baba zao. Baadhi ya akina baba hawajafa, lakini bado hawapo kiroho wala kijamii katika muongozo na mahusiano chanya na watoto wao wenyewe.

Waefeso 6:4 na Wakolosai 3:21 tulizosoma ni ufupisho wa Agano Jipya kuhusu wajibu wa wazazi, hususani upande wa akina baba, kuwafundisha watoto wao Neno la Mungu. Angalia Kumbukumbu la Torati 6: 1-2, 4-8.

> Na hii ndiyo sheria, na amri, na hukumu, alizoziamuru Bwana, Mungu wenu, mfundishwe, mpate kuzitenda katika nchi ile mnayoivukia kuimiliki; upate kumcha Bwana, Mungu wako, kushika amri zake zote, na sheria zake, ninazokuamuru, **wewe** na **mwanao**, na **mwana wa mwanao**, siku zote za maisha yako; tena siku zako ziongezwe… Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa

> bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako.

Sio wakati wa dini ya Kiyahudi au hata wakati huu wa Ukristo ambapo baba angethubutu kupuuzia kuwazoesha (kuwafundisha) watoto wake Neno la Mungu muda wote. Akina baba Wakristo wasiwaachie wake zao peke yao kuwapa elimu ya kidini watoto wao. Pia akina baba kuacha wajibu wao na kutegemea kanisa lichukue wajibu kikamilifu kwa kuwafahamisha watoto wa mtu kuhusus fundisho la Kikristo na maisha ya Kikristo. Ni vizuri kwamba watoto wahudhurie madarasa ya Biblia na ibada kwa masaa machache kila wiki, lakini wazazi wanao watoto kwa masaa yote kila siku. Chukulia madhara mabaya ya kidunia juu ya watoto wetu, wazazi wanapaswa kuchukua kila fursa iliyopo kwa ajili ya uimarishaji chanya wa Biblia.

## Hitimisho

Majukumu ya kanisani na hata majumbani ambayo Mungu aliyaanzisha tangu mwanzo wa safari ya binadamu hapa duniani, bado yanafanya kazi. Mtume wa Mungu Paulo alifundisha wazi wazi kwamba, wajibu huu Mungu aliowapa wanaume na wanawake tangu uumbaji na kuendelea, ulikuwa bado unafanya kazi hata wakati huu wa Ukristo. Hakuna kifungu sehemu yoyote katika Agano Jipya kinachopinga majukumu haya yaliyotolewa na Mungu ya wanaume na wanawake. Hakuna mtu mwenye mamlaka ya kufuta amri ya Mungu iwe katika jambo hili (au lingine) ambalo ameliamuru katika Biblia (Kumbukumbu 4:2; Mithali 30:6; Ufunuo 22: 18, 19).

Ukweli kwamba wanaume wengi wanaweza wasijitokeze kwenye tukio la kuwa “waume” na “akina baba” katika majumba yao, ambavyo wanapaswa kuwa, ni habari ya kusikitisha kwa wanaume, lakini mapungufu hayo ya kibinadamu hayabadilishi kitu, kwa mfano, hayamfanyi “mke” kuwa “mume” wala hayamfanyi “baba” kuwa “mama”. Nyumbani panahitaji majukumu yote, ya mke na ya mume pia yaweze kupangiliwa kama Mungu alivyokusudia pawe.

Wanaume na wanawake wanatofautiana kimaumbile au kiutendaji, lakini wana thamani sawa kwa habari ya wokovu (Galatia 3:27-29). Hata hivyo, Mungu alitoa majukumu tofauti lakini yanayohitajiana kwa wanawake na wanaume. Zingatia majukumu hayo yanayotofautiana, mwanamke anawajibika kumtii mwanamume, mwanamume ana wajibu wa ziada kwa mwanamke. Mungu aliruhusu tofauti hizi za kimaumbile kwa jinsia hizi ili ziendane na majukumu yao husika kwa kila jinsia. Mwanaume anahitaji kutumia nguvu nyingi wakati mwanamke katika majukumu yake ya kumsaidia mara nyingi hayahitaji nguvu.

Wanawake wanaonyesha uwezo sawa wa kielimu na wanaume. Kihisia wanawake wanatofautiana kabisa na wanaume. Katika jinsia hizi mbili, sifa zao za kihisia zikiwekwa pamoja pale nyumbani panakuwa bora sana. Jinsia zote mbili zina uwezo wa kufanya vizuri kitabia, ingawa mara nyingi wanawake hung’aa zaidi ya wanaume. Wapo wanawake ambao kiroho ni mabingwa na ambao wamefanya nyumbani kwetu na Kanisani pawe vile Mungu alivyotaka pawe. Hata hivyo, Si wanawake wala wanaume, watakaokuwa mabingwa kiroho ikiwa hawataheshimu majukumu ya wanamume na wanawake yaliyotolewa na Mungu.

Tukiachilia Mungu Baba, wengine wote wako chini ya wengine (1 Wakorintho 15:24-28; Waebrania 2:8). ***“Lakini nataka mjue ya kuwa,***

***kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha kila mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu"*** (1 Wakorintho 11: 3).

Haipingiki kabisa kwamba Biblia inafundisha wazi wazi kuwa wanawake wako chini ya wanaume (1 Timotheo 2:12; 1 Wakorintho 11:3). Zaidi sana Maandiko yameweka wazi kwamba wanawake wanatakiwa kuwatii waume zao wenyewe (Waefeso 5:22-25; Wakolosai 3:18; Tito 2:5; 1 Petro 3:5-6), hata kama hao waume zao sio Wakristo (1 Petro 3:1).

Majukumu ya wanawake makanisani au hata majumbani yanachanganya kwa wale tu ambao wanaipa heshima ndogo mamlaka ya Mungu na Neno lake takatifu. Wakristo wanaokataa majukumu ya mke kumsaidia mumewe wanapinga *"**mafundisho yenye uzima**"* (Tito 2:1, 4-5) na *"**Wanalitukana Neno la Mungu"*** (Tito 2:5)! Wanaume wanaoshindwa au kupuuza kulibeba mabegani mwao jukumu ambalo Mungu amewapa pia wanapinga Mafundisho yenye uzima na wanalitukana Neno la Mungu.

Neno la Mungu linatoa sababu kadhaa za wanawake kutii; (1) ***"Kwa maana Adamu aliumbwa kwanza na Hawa baadaye"*** (1 Timotheo 2:13). (2) ***"Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa"*** (1 Timotheo 2:14). (3) ***"Maana mwanaume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume"*** (1 Wakorintho 11: 8). (4) "***Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume"*** (1 Wakorinto 11: 9). Lakini bado wokovu wa mwanamke na thamani yake havikufungwa kwa mwanamume (Wagalatia 3:28). Na bado, Injili haipuuzi tofauti baina ya rangi, siasa hali za kiuchumi, au jinsia.

Kutokukubaliana hakuko na mimi, bali na Mungu mwenyewe, pale mtu anapotoa wazo la kubadilisha majukumu husika ya wanawake na wanaume ambayo Mungu aliyaanzisha katika Bustani ya Edeni. Bila shaka tunaweza kuona ubatili wa kubishana na Mungu. Tafadhali tofautisha maudhi yoyote ya ujumbe na mtumaji – Mungu.

# Wajibu wa Wanawake:

*Katika Kanisa*

*Nyumbani*

*Kazi za Kufanya*

**Bonnie Rushimore**

# Wajibu wa Wanawake katika Kanisa

## Ufafanuzi wa Maneno

Tunapojadili kuhusu "wajibu wa mwanamke," kuna maneno matatu ambayo yanawaudhi wale wanaotamani kuyabadili mafundisho ya Biblia yanayohusu wajibu wa mwanamke. Hivyo kabla ya kuirudia Biblia ni lazima tuelewe maana ya maneno haya matatu – usikivu, utii wajibu – kama yalivyotumika tunapoelezea shauku ya Mungu kwa ajili ya "wajibu wa mwanamke." Wanaume na wanawake watakapoelewa namna ambavyo haya maneno yanatumika katika kuyafanyia kazi kibiblia kuhusu wajibu wa mwanamke, mabishano yatakoma, maadam tu Wakristo wanatamani kumpendeza Mungu kwa hakika.

### Usikivu

Maelezo ya kamusi kuhusu "utii" ni "1. Tendo la kutii. 2. Hali au ukweli wa kuwa chini ya." Maneno "chini ya" kama yalivyotumika kwenye fafanuzi iliyopita yako katika kuvumisha, yakimaanisha "kuwa chini ya utawala, udhibiti au ushawishi." Kimsingi, inamaana mtu au kitu fulani kina udhibiti au ushawishi juu yako. Katika siku za uhai wetu, kila mmoja wetu anawajibika kwa mtu au kitu fulani.

### Utii

Utiini nomino ikimaanisha, "1. Kitendo au uwakilishi. 2. Kitu kilichojitoa; pendekezo au hoja, nk. 3. Sifa au hali ya kujiweka chini ya mwingine." Kimsingi neno kuu "kutii" ni kitenzi chenye maana ya, 1.

Kujiweka au kujisalimisha kwenye nguvu au mamlaka ya mwingine. Kujiweka kwenye aina Fulani ya matendo au ushawishi.

Kama unavyoona, maneno “utii” na “usikivu” yanaweza kutumika kwa kubadilishana kwa kuwa yana maana moja. Kuwa katika utii au usikivunikumruhusu mtu fulani kuwana udhibiti na mamlaka juu ya mwingine. Weka maelezo haya akilini tunapoangalia vifungu vya Biblia vinavyofundisha wajibu wa wanawake katika kanisa, na baadaye tutakapojifunza mpango wa Mungu kwa wanawake nyumbani.

## Jukumu

Neno la tatu tunalotakiwa kulielezani “jukumu.” Katika muktadha wamazingira ya somo letu, neno hili ni nomino likimaanisha, “1. Shughuli kamili au ya kila siku: jukumu la mwalimu katika jamii. 2. Sosholojia, haki, majukumu, na kielelezo cha tabia kinachoendana na hali ya kijamii” (*Dictionary.com*). Tunpoangalia “majukumu ya wanawake” kwa maneno mengine ni “wajibu wa wanawake.” Wajibu wa wanawake ni nini? – ni tabia gani ya kawaida ya wanawake inayotarajiwa kama ilivyoamriwa na Mungu katika maandiko yake matakatifu?

## Uhusiano Wenye Mamlaka

Mungu alitoa majukumu (wajibu) kwa mwanamke tangu uumbaji. Adam aliumbwa kwanza na Hawa akaumbwa baadaye. ***“Kwa maana Adam ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adam hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa***” (1 Timotheo 2:13-14). Jukumu la uongozi limefafanuliwa zaidi na Mungu pale aliposema, “Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala”

(Mwanzo 3:16). Mwanaume anapaswa kumtawala mwanamke. Mwanamke anapaswa kuwa mtiifu kwa mwanaume. Hii haimaanishi kuwa wanaume na wanawake hawako sawa. Wanaume na wanawake wako sawa katika wokovu (Wagalatia 3:28). Wala kuwa mtiifu hakumaanishi kuwa mwanamke ni duni au dhaifu.

Waefeso 5:22-6:5 inajadili kuhusu uhusiano na viwango vya mamlaka:

> "Enyi wake, watiini waume zenukama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake na wao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye aliovyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe. Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa. Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe; wala mke asikose kumstahi mumewe. Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi,

> upate heri, ukae siku nyingi katika dunia. Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana. Enyi watumwa, watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo."

Wake wawatii waume zao. Hii ni sawa na Kanisa kumtii Kristo. Kuwa na uhusiano sahihi, waume ni lazima wawapende wake zao, kama vile Kristo anavyolipenda Kanisa. Watoto wanapaswa kuwatii wazazi wao. Wazazi, hasa akina baba, wanapaswa kuwatendea watoto wao kwa haki na upendo na kuwafundisha njia za Mungu. Walioajiriwa wafanye kazi za waajiri wao kama vile wanafanya kazi kwa ajili ya Kristo.

Zaidi ya yote, wanadamu wote wanaamriwa kuitii mamlaka ya serikali ambayo imewekwa. Yesu alifundisha, ***"Basi mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu"*** (Mathayo 22:21). Paulo, katika uvuvio alionya:

> "Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu, na ile iliyopo umeamriwa na Mungu. Hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu. Kwa maana watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi, wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, nawe utapata sifa kwake. Kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya mema. Lakini ufanyapo mabaya, ogopa; kwa maana hauchukui upanga bure, kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu, amlipizaye kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu. Kwa hiyo ni lazima

> kutii, si kwa sababu ya ile ghadhabu tu, ila ni kwa sababu ya dhamiri. Kwa sababu hiyo tena mwalipa kodi, kwa kuwa wao ni wahudumu wa Mungu, wakidumu katika kazi iyo hiyo. Wapeni wote haki zao, mtu wa kodi, kodi, mtu wa ushuru, ushuru, astailiye hofu, hofu, astahiliye heshima, heshima." (Warumi 13:1-7)

Mungu anatutaka tuonyeshe heshima na utii kwa viongozi wa nchi. Ni lazima tuzitii sheria za nchi tunayoishi au tunayoitembelea. Jambo pekee la kuliangalia katika amri hii ni pale baadhi yasheria za nchi zinapopingana na sheria za Mungu (Matendo 5:29).

Vifungu hivi vya maandiko vinaonyesha wazi kuwa katika kila hatua ya maisha kila mmoja wetu ameamriwa kumtii mtu mwingine. Kila mtu mmoja mmoja anapaswa kuwa chini ya mamlaka ya mtu mwingine. Watoto wako chini ya mamlaka ya wazazi wao. Wanafunzi wanapaswa kuwatii walimu wao. Wafanyakazi wanapaswa kuwatii mabwana zao [wakuu wao wa kazi]. Raia wanapaswa kutii sheria na kanuni za serikali yao. Tunaelewa kuwa mtu anatakiwa kuwana kauli na mamlaka ya mwisho juu yake. Vinginevyo, tungeishi kwenye ulimwengu wenye machafuko na kuchanganyikiwa kwingi. Sasa,kwanini hatutaki kukubali kuwa kuna mtu ana kauli na mamlaka ya mwisho juu yetu katika dini? Vifungu vya maandiko hapo juu vinafundisha wazi kuwa wake wanatakiwa kutii uongozi wa waume zao. Kanisa linamtii Kristo, na Kristo anamtii Mungu Baba – kama ilivyo kwa WANADAMU WOTE.

## Vifungu vya Maandiko Vinavyozungumzia Wajibu wa Wanawake ndani ya Kanisa

***1 Wakorintho 11:2-16***

“Basi nawasifu kwa sababu mmenikumbuka katika mambo yote, nanyi mmeyashika yale mapokeo vile vile kama nilivyowatolea. Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo,na kichwa cha kila mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu. Kila mwanamume asalipo, au anapohutubu, naye amefunikwa kichwa, yuaaibisha kichwa chake. Bali kila mwanamke asalipo, au anapohutubu, bila kufunika kichwa, yuaaibisha kichwa chake, kwa maana ni sawasawa na yule aliyenyolewa. Maana mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele. Au ikiwa ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake au kunyolewa, na afunikwe. Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume. Maana mwanamume hakutoka kwa mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume. Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume. Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani, kwa ajili ya malaika. Walakini si mwanamke pasipo mwanamume, wala mwanamume pasipo mwanamke, katika Bwana. Maana kama mwanamke alitoka kwa mwanamume, vile vile mwanamume naye huzaliwa na mwanamke, na vitu vyote asili yake hutoka kwa Mungu. Hukumuni ninyi wenyewe katika nafsi zenu. Je, inapendeza mwanamke amwombe Mungu asipofunikwa kichwa? Je, hayo maumbile yenyewe hayawafundishi ya kwamba mwanamume akiwa na nywele ndefu ni aibu kwake? Lakini mwanamke akiwa na nywele ndefu ni fahari kwake. Kwa sababu amepewa zile nywele

ndefu ili ziwe badala ya mavazi. Lakini mtu ye yote akitaka kuleta fitina, sisi hatuna desturi kama hiyo, wala makanisa ya Mungu."

Katika sura hii Paulo alielezea mpangilio wa uongozi – huo ulianzishwa katika uumbaji – pia anaelezea namna uhusiano unavyokuwa katika majukumu. Neno "kichwa" linamaanisha mamlaka au nafasi ya juu ya uongozi. Wanawake wako chini ya mamlaka ya wanaume, wanaume wako chini ya mamlaka ya Kristo na Kristo yuko chini ya mamlaka ya Mungu. Mistari wa nane na wa tisa inaelezea sababu ya mpangilio huu kimajukumu – mwanamke aliumbwa kutoka kwa mwanamume,tena mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanamume (linganisha na Mwanzo 2:20-23). Kama tulivyoona, kwa mmoja kuwa chini ya mamlaka ya mwingine haimfanyi kuwa mnyonge kwa mwingine.

Kirai "kwa sababu ya malaika" kinaonyesha matokeo ya wanawake kutotii mamlaka ya Mungu kuwa wawe watiifu kwa wanaume. Malaika waliposhindwa kufuata mpangowauongozi wa Mungu, walitupwa katikavifungo vya milele chini ya giza (Yuda 6). Wanaume, wanawake na malaika wanapaswa kufuata amri zote za Mungu na kuzifanyia kazi, zikiwepo kanuni zake za utii/mamlaka. Kushindwa kufanya hivyo kutaleta matokeo ya umilele usio na furaha.

Pauloalipowakuwakumbusha Wakorintho juu ya mpangilio wa uongozi, alianza mjadala wake wa sala na kutoa unabii. Neno la Kiyunani kwa mwanamume ni *aner*, likimaanisha "jinsia ya kiume" – halijawahi kufasiriwa 'mwanadamu,' ambalo lingewahusisha wanawake pia. Kuhusu sala na unabii, Paulo anawazungumzia wanaume. Maelezo ya kwanza ya nomino ya Kiyunani kuhusu "nabii" inamaanisha kusema fikrana mausia ya Mungu…" na maana ya kwanza ya Kiyunani ya kitenzi "tabiri" ni kuwa nabii, kutoa unabii, limetumika

likiwa na maana ya awali ya kutoa unabii juu ya mausia Matakatifu… (Vine).

Don Mc Whorter alichunguza yafuatayo:

> Suala juu ya uongozi wa jinsia ya kiume na utii wa jinsia ya kike limeelezewa kwa uwazi na kwa nguvu kabisa. Paulo anaweka hali ya kinadharia katika mstari wa 4 na wa 5 kulielezea hili. Katika utamaduni wao kutofunika kichwa kuliashiria utawala, wakati kufunika kichwa kulionyesha utii. Katika mstari wa 4 anaelezea kanuni ya utawala kwa kutumia hali ya kufikiria ya kile ambacho mwanaume wa utamaduni huo asingeweza kamwe kufikiria kufanya hivyo – [mwanaume] kusimama na kuongoza mkusanyiko akiwa amefunika kichwa…aliendelea na kielelezo, anajenga hoja katika mstari wa 5 kwamba mwanamke asithubutu kufanya kile ambacho mwanaume asingeweza hata kufikifikiria kuwa kingefanyika… Katika jamii ile, utii wa mwanamke ulionekana kwa kufunika kichwa. Angethubutuje kuacha wajibu wake wa kutii! Angefanya hivyo kama angetaka kujionyesha akiwa hajafunika kichwa chake.

Mistari hii inafundisha wazi kwamba mwanamke hawezi kuwa na jukumu la kumwongoza mwanaume na wakati huo huo kuwa mtiifu kwake. Hali hiyo haiwezekani!

Urefu wa nywele uliozungumziwa katika mistari wa 14 na 15 unataja tena uhusiano wa mamlaka/utii. Desturi katika kipindi cha uandishi huuni mwanaume kuwa na nywele fupi na mwanamke kuwa na nywele ndefu.  Nywele fupi kwa mwanaume ziliashiria mamlaka wakati nywele ndefu na kilemba kwa mwanamke villiashiria utii. Ikiwa mwanamke atakata nywele au kuvua kilemba aliwaonyesha wale waliomwona kuwa si mtiifu tena kwa uongozi wa wanaume. Wakati

Biblia haitaji "urefu wa nywele unaotakiwa" na "ufupi wa nywele unaotakiwa" kulingana na nywele za mwanaume na mwanamke, mtoto ye yote wa Mungu akiwa na shauku ya kumpendeza Baba ataangalia urefu na mtindo wa nywele, uchaguzi wa mavazi, pamoja na mwenendo wa maisha ya kila siku sambamba na utamaduni wa jamii ambayo mtu husika katika hiyo au anaitembelea. Je, mwanamke aliye na nywele fupi, mtindo wa nywele wa kiume anaonyesha tabia ya utii katika uongozi wa mwanaume?

***1 Wakorintho 14:34-35***

> "Wanawake na wanyamze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena bali watii, kama vile inenavyo torati nayo. Na wakitaka kujifunza neno lolote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu mwanamke kunena katika kanisa."

Mazingira ya 1 Wakorintho 14 nimkusanyiko wa ibada. Kuanzia mstari wa 26, Paulo anazungumzia matumizi ya lugha katika ibada. Kama hakuna mtu wa kufasiri, yule anayenena kwa lugha ngeni aliambiwa anyamaze. Nabii alipotaka kuleta ujumbe kutoka kwa Mungu, Paulo alimwambia asubiri zamu yake. Yule anayenena alitakiwa amalize somo lake, ili awape wengine nafasi ya kunena (mst 29-32), kwa hivyo, wote waliohudhuria walipata nafasi ya kujifunza. Mtume Paulo, kwa uvuvio wa Roho alilisihi kanisa la Korintho kuruhusu mtu mmoja anene kwa wakati wake. Hatuwezi kujenga (26) ikiwa watu kadhaa wananena kwa wakati mmoja. Mstari wa 40 unasema, "lakini mambo yote yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu." Mistari ya 34-35 inafundisha kuwa wanawake hawaruhusiwi kusema neno katika mkusanyiko wa hadhara. Muktadha katika mistari hii miwili unalenga hasa kuongoza nyimbo na sala pamoja na kuhubiri mbele ya wanaume.

Zaidi ya yote, mtume alithibitisha kwamba vilevile kanuni hii ilikuwa maridhawa au muhtasari wa hisia za Agano la Kale kwa ujumla. Hakuna kifungu maalum ambacho kina kirai kinachosema “pia sheria imesema” rejea, lakini marejeleo ni sheria ya Mungu ya Agano la Kale . Hata hivyo, majukumu ya heshima yaliyowekwa na Mungu ya mwanaume na mwanamke, tangu uumbaji tunaposoma katika Biblia, si magumu kuyafuata. Kimsingi, mtume Paulo anawakumbusha wasomaji wake kuwa sheria ya Mungu kuhusu nafasi husika na tofauti ya wanaume na wanawake haijabadilika kutoka Agano la Kale kwenda Agano Jipya.

Don McWhorter anatoa fafanuzi ndogo yenye tofauti ya kirai ***“kama vile inenavyo torati”*** (mstari wa 34):

> …ni sheria ya utii ambayo Paulo anasema ilithibitishwa na “sheria.” Amri ya kunyamaza kwa wanawake katika hali inayojadiliwa ilikuwa ni matumizi ya sheria ya utii. Maneno ya Paulo ni “wameamriwa kuwa watii, kama inenavyo torati.”

Ama Paulo alikuwa akirejelea sheria ya Agano la Kale la Mungu” au zaidi hasa katika “sheria ya utii” isiyo na maana, kwa kuwa sheria ya Mungu ya utii ilianza katika Bustani ya Eden hapo mwanzo wa wakati. Mpango wa Mungu wa kutenganisha wajibu wa wanaume na wa wanawake haujabadilika tangu uumbaji hadi sasa.

Hata hivyo, mtu anapaswa kukumbuka kuwa wanawake wameamriwa kumwimbia Mungu katika ibada, na mstari huu hauwazuii kuimba. Kifungu hiki kinawakataza wanawake kuchukua jukumu la kuongoza – kujiweka katika nafasi ya kuwatawala wanaume – katika mkusanyiko wa hadhara.

Labda mwandishi aliyevuviwa alijua kuwa wengine watapinga mjadala huu kuhusu wajibu wa wanaume na wanawake katika mkusanyiko wa hadhara. Zingatia mstari wa 37, “mtu akijiona kuwa ni nabii, au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya

kwamba ni maagizo ya Bwana." Paulo alishauri kuwa wale wanaoamini kuwa na maarifa ya kimungu wanapaswa wathibitishe kuwa maelezo haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu.

***1 Timotheo 2:8-12***

> "Basi nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano. Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu. Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanaume, bali awe katika utulivu."

Mazingira ya 1 Timotheo 1:8-12 yanahusu ibada na kubainisha majukumu husika ya wanaume na wanawake kuhusu nyanja yake ya wazi. Katika 1 Timotheo 2, Paulo ametumia maneno tofauti tofauti ya Kiyunani alipokuwa akizungumzia wanaume na wanawake. Katika mstari wa 8 na wa 12, ametumia neno *aner*, likimaanisha "mwanaume mmoja mmoja," alipokuwa akiwaelekeza wanaume. Alitumia neno *gune* katika mstari wa 9 na wa 12 akimaanisha "mwanamke;hasa mke," alipokuwa akiwataja wanawake. Mwanzoni mwa sura (mistari ya 1,4-5), mtume Paulo alitumia neno *anthropos*akimaanisha wanadamu, alipokuwa akitoa maelekezo yale yale kwa wanaume na wanawake.

Neno la Kiyunani la "kimya" ni *hesuchia*likimaanisha "utulivu" [kuacha, kutoka katika kitendo, kuacha au kuepuka]zogo au lugha: utulivu, ukimya." Neno ukimya limatumika mara mbili katika mazingira haya, mara zote likiwahusu wanawake. Wanapaswa kujifunza kwa

utulivu, na wanatakiwa kujizuia kuwafundisha na kuwatawala wanaume. Kwa uwazi kabisa mwandishi aliyevuviwa kwa makusudi kabisa alichagua maneno tofauti tofauti kuwafundisha wanaume na wanawake akiwaonyesha majukumu na tabia tofauti katika kumwabudu Mungu.

Katika sehemu hii ya maandiko, Mungu aliwaamuru wanaume kuongoza sala katika ibada. Hakuna mwanaume atakayempa mwanamke ruhusa ya kuongoza sala wakiwemo wanaume. Wanawake wameamriwa kutowanyang'anya wanaume madaraka. Mwanamke anapoongoza sala mbele ya wanaume, anakuwa amewanyang'anya wanaume mamlaka na kutawala yeye.

Jane McWhorter alibainisha:

> Mwanamke …Hakuwahi kupewa haki ya kumfundisha mwanaume katika hali ya utawala. Kanuni hii pana inatumika popote pale ambapo Wakristo wamekusanyika kwa kusudi la kiroho, ikiwa ni katika jengo la kanisa, nyumbani, ukumbini, au hadharani katika chuo cha Wakristo. Hakuna mwanaume, hata mzee, anayeweza kumpa mwanamke ruhusa ya kuvunja sheria ya Mungu.

Hata hivyo, wanawake wameamriwa kumwimbia Mungu katika ibada (Waefeso 5:19). Kulingana na Wakolosai 3:16 nyimbo tunazoimba ni za kufundishana na kuonyana sisi kwa sisi. Hivyo, wanawake wanapoimba nyimbo za kumsifu Mungu, wanawafundisha wanaume ambao nao pia wanamwimbia Mungu nyimbo za sifa.

Zaidi ya yote, ulinganifu umewekwa kati ya mwanaume anavyotakiwa kusali na kumtumikia Mungu na namna ambavyo mwanamke mcha Mungu anavyotakiwa kutenda. Mwanamke mcha Mungu anajulikana kwa namna anavyovaa. Anajali sana mavazi ya

kiroho kuliko mavazi ya kimwili. Tunapojitahidi kujaribu kutumia sifa za kimungu katika maisha yetu, tutakuwa na mavazi bora ya kiroho.

Hakuna mbadala kwa mwanamke mcha Mungu katika kanisa. Nafasi yao ya huduma ya utii ni muhimu katika kanisa na ya thamani sana katika kukua kwa kanisa. Wamebarikiwa na wajibu wa kuendelea "katika imani na upendo, na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi" (1 Timotheo 2:15). Msaada, uelewana sifa zinafaa katika "kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwasukwa hata kumwagika" (Luka 6:38) maana kima chake chapita kima cha marijani."

Biblia inasisitiza kuwa wanawake wanapaswa wawatii wanaume. Wanawake hawawezi kuhubiri, kusali au kuongoza nyimbo, au kuhudumia Meza ya Bwana, au kufundisha darasa la Biblia, au kutumika kwa namna yoyote ile kunakoonyesha kuwa na mamlaka juu ya wanaume. Mwanamke ye yote Mkristo mwenye shauku ya kumtumikia Bwana wake kwa upendo kabisa atakubali agizo la Mungu la uongozi. Atatii kwa unyenyekevu uongozi wa wanaume kanisani na nyumbani. Atakuwa mtiifu – si kwa sababu anatakiwa kufanya hivyo – bali kusudi awe mtumishi mwaminifu kwa Bwana wake.

## Swali

1. Je, kuna mazingira yoyote yanayompa mwanamke ruhusa ya kumfundisha mwanaume?

# Wajibu wa Wake katika Nyumba

Tumeshajadili kuhusu maana ya maneno "chini ya" "utii" na "jukumu." Uelewa wa wazi wa maneno haya unahitaji kufahamu mpango wa Mungu kwa wanaume na wanawake. Kama ukumbusho – kuwa "chini ya" na "utii" yana maana moja kimsingi "kuwa 'chini ya' au kuwa katika hali ya 'utii'ni kumruhusu mtu kutawala na kuwa na mamlaka juu ya mwingine." Neno "jukumu" linafanana na "wajibu." Hivi, Biblia inaeleza nini kama "wajibu wa wake katika nyumba?" Natumia neno "wake" kwa kuwa mwanamke ambaye hajaolewa, anayeishi peke yake, ni kichwa cha nyumba yake kwa kuwa ni yeye mwenyewe anayeishi pale.

## Maandiko Yanayozungumzia Majukumu ya Wake Ndani ya nyumba zao

***Mwanzo 2:15-25***

> "Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, matunda ya kila mti wa bustani waweza kula. Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika. Bwana Mungu akasema, si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa mwituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake. Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa

> kufugwa na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Adamu akasema, sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume. Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya."

Hapo mwanzo Mungu aliumba ulimwengu uliokamilika. Baada ya Adamu kuwapa majina wanyama wote hakupatikana msaidizi kwa ajili yake (Mwanzo 2:20). Mungu alimuumba msaidizi maalum kwa ajili ya Adamu kutoka katika ubavu wa Adamu. Mungu alipanga tangu mwanzo kuwa mwanamume atakuwa na mwenzi wake wa kumsaidia. Ni muhimu kujua kuwa Hawa aliumbwa kutoka katika ubavu waAdamu. Hakuumbwa kutoka katika mfupa wa mguu wake ili amkanyage au kutoka katika kichwa chake ili amtawale [yaani atawaliwe Adamu], bali kutoka katika upande wake ambao anaweza kumlinda na yeye[mke] aweze kumsaidia.

***Mwanzo 3:16***

> "Akamwambia mwanamke, hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala."

Baada ya dhambi ya Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni, Mungu alitangaza adhabu kwa kila mmoja wao. Adamu aliambiwa kuwa atakula kwa jasho, na michongoma na miiba itamzalia, na Mungu akawafukuza watoke katika Bustani ya Edeni.

Hawa alipewa adhabu iliyozidi. Aliambiwa atapitia uchungu zaidi atakapokuwa akizaa watoto, na tamaa yake itakuwa kwa mumewe. Adamu alitakiwa kumtawala. Adhabu hizi zinaendelea katika kila kizazi tangu kipindi hicho maadam tu ulimwengu ungalipo. Wanawake wote tangu kipindi hicho na kuendelea wanatakiwa kuwa watiifu kwa waume zao.

***Waefeso 5:22-6:5***

> “Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno, apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe tukufu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mke wake hujipenda mwenyewe. Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye alivyolitendea kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila

> mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa. Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe; wala mke asikose kumstahi mumewe. Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, upate heri, ukae siku nyingi katika dunia. Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana. Enyi watumwa, watiini wao walio bwana zenu kwa jinsi ya kimwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo."

Mtume alieleza kuwa kama vile Kristo alivyo kichwa cha Kanisa, mume naye ni kichwa cha mke. Katika uhusiano huu, Kanisa linapaswa kumtii Kristo na mke anapaswa kumtii mume wake. Paulo aliendelea na ulinganifu huo huku akiunganisha upendo ambao Kristo anao kwa ajili ya kanisa na upendo mume anaopaswa kuwa nao kwa mke wake. Kwa kawaida, wanaume wanaijali na kuilisha miili yao, na Paulo anaeleza kuwa mume anayempenda mke wake kwa dhati atamtendea kama anavyojitendea mwenyewe. Mume atamlisha na kumthamini mke kama atakavyojifanyia mwenyewe. Mume anapomtendea mke wake kama anavyopaswa kutenda, mke kwa upendo na hiari atafuata amri ya Mungu ya kuwa mtii kwa mume wake.

Kwa bahati mbaya, wanaume wengine husahau kuifanyia kazi wakiwatendea vibaya wake zao. Hivyo, ni vigumu kwa mke kuwa na utii sahihi kwa mume wake. Hata hivyo mwanamke bado anatakiwa kumtii mume wake hata kama mume hamtendei kama Mungu alivyomwamuru. Jambo pekee ambalo mke hatafanya katika kutekeleza sheria hii iliyotolewa na Mungu ni pale mume anapomtaka mke afanye jambo ambalo ni kinyume na sheria ya Mungu

(Kumbukumbu 13:6-8; Mathayo 19:29; 10:37; Matendo 5:29). Ingawa hatuishi chini ya sheria ya kale, kanuni haijabadilika. Mungu hatakubaliana na visingizio siku ya hukumu, "nilipaswa kumtii mume wangu." Wala hatakubaliana na kisingizio cha, "mume wangu hakunijali, ni mkali na ni katili (au sifa yoyote mbaya)."

Kama mke, mwanamke ni zaidi ya mwenzi. Mke ni mshirika wa mume wake katika jitihada zao za pamoja katika malengo ya hapa duniani na ya mbinguni, kupitia majukumu yanayotofautiana. Mke mwaminifu na mwajibikaji anastahili upendo na kutendewa wema na mume wake (Wakolosai 3:19; 1 Petro 3:7). Akila na Prisila ni mfano mzuri katika Biblia wa mume na mke ambao wanastahili kuigwa kipindi hiki (Matendo 18:24-26; Warumi 16:3-5).

Waefeso 5:22-6:5 bila kukosea inathibitisha kuwa wake wanapaswa kuwa watiifukwa waume zao. Hii ni sawa na Kanisa kuwa na utii kwa Kristo. Ili kuwana uhusiano sahihi, waume wanapaswa kuwapenda wake zao, kama vile Kristo alivyolipenda kanisa. Watoto wawe watiifu kwa wazazi wao. Wazazi, hasa akina baba, wameamriwa kuwatendea watoto haki nakuwa na upendo kwao wakiwafundisha njia za Mungu. Waajiriwa wawafanyie kazi waajiri wao kama vile wanamfanyia Bwana.

***Tito 2:3-5***

> "Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema; ili wawatie vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao, na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe."

Tito sura ya pili inatoa muhtasari wa sifa na wajibu wa Wakristo. Mstari wa kwanza unawaelekeza wazee [viongozi], mstari wa pili unafundisha wazee [wanaume] wa makamo, mistari ya 3-5 inawahusu wanawake wazee, mistari ya 4-5 inawahusu vijana wa kike, mstari wa sita unawahusu vijana wa kiume na mstari wa 9 unatoa maelekezo kwa watumwa (leo unawahusu wafanyakazi). Katika mazingira haya, wanawake wazee wanatakiwa kuwafundisha wanawake vijana "kuwapenda waume zao, kuwapenda watoto wao, kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao." Wanawake wazee hawataweza kufundisha sifa hizi kwa wanawake vijana ikiwa hawaelewi au hawana sifa hizi katika maisha yao.

Zoezi la ndoa za kitamaduni lililofanyika kipindi cha uandishi wa kitabucha Tito lilikuwa la ndoa zilizopangwa. Vijana wa kiume na wa kike hawakuwa na uhuru wa kuchagua wenzi wao; wazazi wake [kijana wa kiume] waliomba kupata mwenzi kwa ajili ya mtoto wao. Kwa kulijua hili inampa mtu uelewa mzuri kwambani kwanini wanawake wazee walitakiwa kuwaelekeza wanawake vijana kuwapenda waume zao na kuwapenda watoto wao.

Ebu tuziangalie kwa karibu sifa za mwanamke Mkristo kama ilivyoanishwa katika mistari hii. "wawapende waume zao" – *philandros* "mpende mtu, ambayo ni mwenye mapenzi kama mke." Mwenye mapenzi ina maana ya kuonyesha, kuashiria, yenye sifa za mapenzi; ya kupendeza; kukumbatiana kwa upendo." Mke anapaswa kuonyesha mvuto wa kimwili na kumsikiliza mume wake.

"Kuwapenda watoto wao"- *philoteknos* "mtu kuwapenda watoto, ambao ni upendo wa mama." Upendo ambao mke anao kwa mume wake na upendo ambao anao kwa watoto wake ni tofauti.

Wanawake wanapoonyesha upendo kwa waume na kwa watoto, upendo kwa mume unapaswa kuwa wa ya kimwili.

“Kuwa wenye kiasi” – *sophron* “kuwa wenye fikra sahihi akilini mwao, enye kujidhibiti (walio na wastani katika maoni au shauku).” Wanawake wanapaswa kuwa sawa, wakidhibiti na kuzuia matendo na hisia zao.

“Kuwa safi” – *hagnos*“jinsi ipasavyo, safi, (ni lugha ya mfano) asiye na hatia, mwenye kiasi, mkamilifu.” Matendo ya wanawake Wakristo siku zote yanatakiwa yawafanye waonekane watu wasio na hatia na wenye kiasi, wasiwe wachafu, wala wabaya [katika mwenendo wao], au wasiofaa.

“Kufanya kazi nyumbani mwao” – *oikourgos* or *oikouros* “anayekaa nyumbani, mwenye mwelekeo wa ndani (anayetunza nyumba yake).” Ni wajibu wa mwanamke kuitunza nyumba yake. Hakika Mungu amewapa wanawake kazi ya kufanya, (1) ambayo wanatakiwa waikubaliiili kumpendeza [Mungu], (2) ambayo inatakiwa ipokelewe kwa upendo na (3) ambayo katika hiyo wanawake wanastahili kushukuriwa kwa kazi yao ya uchaji wa Mungu. Cindy Colley alifanya uchunguzi: “. . . usahihi wa kirai “wanaofanya kazi nyumbani mwao” unataka uelewa wetu. Kama vile mlinzi wa bustani [ya wanyama] anavyofanya kazi katika bustani, vile vile “anayefanya kazi nyumbani” anahakikisha anafanya kazi zote za nyumbani.”

“Kuwatii waume zao wenyewe”–*hupotasso* “kuwa chini; kuwa wenye kutafakari, kutii.” Wanawake wanatakiwa wawatii waume zao. Kama tulivyoona kwenye mistari iliyopita, amri ya Mungu kwa wanawake kuwatii waume zao inaturudisha kwenye uumbaji. Wanawake wakishindwa kuwa watii kwa waume zao, wanamchafua au kumsema Mungu vibaya.

Hizi ni baadhi tu ya sifa za wanawake wote, vijana na wazee, wanapaswa wajitahidi kuziendeleza katika maisha yao ya kila siku. Mtu anapozifanyia kazi sifa hizi katika maisha yake ya kila siku, nyumba itakuwa yenye upendo, amani, na yenye kujitenga na maovu ya dunia hii.

***1 Timotheo 5:14***

> "Basi napenda wajane, ambao si wazee, waolewe, wazae watoto, wawe na madaraka ya nyumbani; ili wasimpe adui nafasi ya kulaumu."

Muktadha wa mstari huu unahusu wajibu wa kuwatunza wajane. Kanisa limeelekezwa kuwajali wajane walio wazee ambao hawana watu wa kuwatunza, endapo watakuwa na sifa zinazotakiwa. Kanisa halitakiwi kuwatunza wajane vijana, kwa kuwa kufanya hivyo kutawafanya wawe wavivu, na kutoa nafasi kubwa zaidi ya majaribukatika dhambi. Ingawa sehemu hii ya maandiko inawalenga wajane, maelekezo yanaweza kuwahusu wanawake wote.

Wajane vijana wanashauriwa waolewe. Paulo alifundisha kuwa inakubalika kuolewa au kubaki bila kuolewa (1 Wakorintho 7:7-40). Katika mstari wa 34, Paulo anaeleza kuwa mwanamke ambaye hajaolewa atajishughulisha na kazi ya Bwana, wakati mwanamke aliyeolewa atajishughulisha na kumpendeza mume wake. Hakuna atakayehukumiwa si aliyeolewa au ambaye hajaolewa.

Wanawake wanashauriwa wawe na watoto. Kuna tofauti kubwa kati ya kuzaa watoto na kuwa mama. Waefeso 6:4 inawaamuru akina baba kuwalea watoto wao katika adabu na maonyo ya Bwana. akina mama wanatakiwa kusaidia katika maelekezo haya. Kumbukumbu 11:19 inasema, "***Nayo wafunzeni vijana wenu kwa kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na***

***uondokapo***." Mafundisho ya Biblia ni tukio la siku nzima na kila siku. Mafundisho haya si ya kukaa darasani tu, bali yanapaswa kufundishwa siku nzima katika shughuli za kawaida pia. Zungumza na watoto wako kuhusu Mungu wa viumbe unapotembea nje na kuona maajabu ya dunia hii. Zungumza na watoto wako kuhusu njia za kimungu za kukaa na wengine pale kutokukubaliana kati ya marafiki kunapotokea. Waonyeshe watoto wako upendo na wema kwa kuwahusisha katika kuandaa na kuwapelekea chakula wagojwa, wafiwa, na waliofungwa. Mtu mwenye hekima Sulemani alifundisha, "***Mlee mtoto katika njia ipasayo naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee***" (Mithali 22:6). Kulea ni zaidi ya kufundisha – ni kuweka katika vitendo ukweli unaofundishwa katika Biblia. Ni lazima tuwafundishe watoto wetu maarifa ya Biblia na tuwasaidie wayaweke katika vitendo. Hatuwezi kuwalea watoto wetu wawe watumwa waaminifu wa Bwana ikiwa sisi tumeshindwa kuwa watumwa waaminifu wa Bwana.

Si kwamba tu akina mama wawasaidie akina baba kufundisha watoto neno la Mungu tu, bali pia wanatakiwa wasaidie kuwatia nidhamu watoto wao. Mtoto asiyekuwa na nidhamu hawezikuheshimu mamlaka. Ni lazima watoto wajifunze kuheshimu mamlaka ya wazazi, walimu, sheria za nchi, wazee na viongozi wengine wa kanisa, na Mungu. Sulemani alitangaza, "***Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe, bali yeye ampendaye humrudi mapema***" (Mithali13:24). "***Fimbo na maonyo hutia hekima, bali mwana aliyeachiliwa humwaibisha mamaye***" (Mithali 29:15). Nidhamu sahihi ni katika hali zote mbili chanya na hasi, na lazima itolewe kulingana na umri na tabia ya mtoto. Wakati mwingine kuangalia kwa ukali kunahitajika ili kurekebisha tabia ya mtoto na wakati mwingine au kwa mtoto mwingine hatua kali zaidi zinahitajika. Liliwezekana kwa mtoto mmoja huenda liwezekane kwa mtoto mwingine. Urekebishaji mzuri wa tabia

ya mtoto utaendelea kwa muda mrefu ili umsaidie mtoto kujifunza kujidhibiti.

Kufundisha na kutia nidhamu kunatakiwa kuanza tangu kuzaliwa kwa mtoto. Tabia iliyokubalika jana lakini haikubaliki leo inasababisha mtoto kuchanganyikiwa. Hatujachelewa kuwalea watoto wetu katika Bwana; kulea kunahusisha maarifa ya Biblia, kuyaweka katika vitendo maarifa hayo,na nidhamu.

Paulo alikiri utekelezaji wa Loisi na Eunike alipomwambia Timotheo, "***Nikiikumbuka imani uliyo nayo isiyo na unafiki, ambayo ilikaa kwanza kwa bibi yako Loisi, na katika mama yako Eunike, nami nasadiki wewe nawe unayo***" (2 Timotheo 1:5). Imani kubwa ya Timotheo ilitokana na bibi yake na mama yake. Mafundisho yao ndiyo yaliyomfanya awe imara, na awe mtumwa mwaminifu wa Bwana katika ujana wake.

Mke [chini ya uongozi mume] anatakiwa kuisimamia nyumba. Ni wajibu wake kuhakikisha kwamba familia inahudumiwa vizuri. Aya hii haipingani na aya nyingine zinayofundisha kuwa mume ni kichwa cha nyumba na mke anatakiwa kuwa chini yake. Badala yake, aya hii inatoa ufafanuzi zaidi. Wakati mume ni kichwa cha nyumba, ni wajibu wa mke kuhakikisha ukamilifu wa mahitaji ya kila siku ya familia ndani ya nyumba. Mwanamke ana haki na mamlaka ya kufanya maamuzi kuhusu wajibu wa kuongoza na kutunza nyumba yake. Mume mwenye hekima na mcha Mungu atampa moyo mke wake kwa kutoa maamuzi ambayo yatasaidia kila siku kazi za nyumbani. Atataka ushauri wa mke wake katika mambo yote yanayohusu familia. Mke mwenye hekima na mcha Mungu atayafanya majukumu yake nyumbani, akimshirikisha mume wake kabla ya kufanya maamuzi yaliyo makubwa. Atakuwa mwenye maarifa juu ya mambo ya nyumbani na ya duniani ili kwa hekima aweze kuzungumza na mume wake mambo ya kifamilia. Mke

mcha Mungu kwa hiari atajishusha katika maamuzi ya mume wake hata kama hakubaliani naye.

***1 Petro 3:1-6***

> “Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu, kusudi ikiwa wako wasioliamini neno, wavutwe na mwenendo wa wake zao, pasipo lile neno, wakiutazama mwenendo wenu safi na wa hofu. Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani kusuka nywele, na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi, bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika, yaani roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao. Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yoyote.”

Hili ni fungu linguine la maandiko – wakati huu limeandikwa na mtume Petro akiwaelekeza wake wawatii waume zao. Petro alielekeza zaidi kuwa hata kama mume si Mkristo, inampasa mke abaki kuwa mtiifu kwake. Ikiwa mke atamtanguliza Mungu katika maisha yake, atakuwa mtiifu kwa mume wake na atatenda kama mtoto mwaminifu wa Mungu, kuna uwezekano mkubwa kuwa mume ataweza kuitii injili. Wanawake Wakristo inawapasa kujali sana kile kilichomo ndani [rohoni] kuliko kile wanachovaa nje. Muda na fedha zilizotumika katika mitindo ya nywele, vito vya thamani na nguo vinaweza kuunganishwa kwa karibu sana na mahali moyo ulipo. Petro hakuwahukumu wake waliovaa ili wawavutie waume zao. Alikuwa analinganisha kati ya wale ambao wanajali zaidi muonekano wa nje kuliko tabia ya kimungu.

Kuvaa kwetu kusiwe kitu cha kwanza ambacho watu watakigundua kwetu. Wakati Fulani, tunapojitahidi kuonyesha kuwa na sifa zinazofanana na Kristo hadharani, tunakosea kwa kufikiri kuwa hakuna anayetugundua kama hatuonyeshi tabia nzuri nyumbani. Usisahau kuwa waume na watoto wetu mara zote wanatutazama. Katika mazingira ya sehemu hii ya maandiko, ambapo mume si Mkristo, ni muhimu sana kuwa tabia zetu za kimungu zionekane nyumbani.

Tafadhali zingatia vipengele hivi ukivilinganisha na kirai ***“kama Sara alivyomtii Ibrahimu akamwita bwana.”***

- Alimtambua Ibrahimu kama kichwa cha nyumba na wa kwanza moyoni mwake.
- Alionyesha kuwa anatambua nafasi yake nyumbani mwake na katika maisha ya Ibrahimu. Aliona ukamilifu ndani yake.
- Alifurahia kuwa mwanamke, mke wa Ibrahimu, na alipata furaha katika upendo wake kwa Ibrahimu.
- Alionyesha upendo mkubwa kwa Ibrahimu.
- Alionyesha upole moyoni mwake kwa ajili ya Ibrahimu.
- Alionyesha namna anavyoona fahari kwa ajili ya Ibrahimu, na alifurahia kuwa mke wake.
- Alionyesha heshima na pongezi kwa Ibrahimu.

Unamwitaje mume wako? Jinsi unavyozungumza naye na unavyozungumza kuhusu mume wako unawaonyesha wengine hisia ulizonazo kwake. Je, wengine wanaweza kuona upendo na heshima ambayo mume wako anastahili kwa maneno na matendo yako, au wanaona kutojali, dharau au chuki? Hili linahusika si kwa waume tu, bali kwa wote tulio na uhusiano nao wa karibu (watoto, wazazi, marafiki, n.k).

# Majukumu ya Wanawake Nyumbani

Wanawake wote wanapaswa kuonyesha upendo na heshima kwa waume zao na kwa watoto wao. Wanawake wanapokuwa wa upendo na heshima sahihi kwa watu wa familia zao, kuwajali itakuwa furaha na wala si mzigo.

Ni wajibu wa mwanamke kuisimamia na kuijali nyumba yake. Nyumba inayotunzwa vizuri itakuwa safi na imepangiliwa. Hata hivyo, haiwezekani kuwa haina doa au kitu kutokuwa mahali pake-itaonekana kuwa "watu wanaishi." Hata hivyo haipaswi kuwa na uchafu wa juma zima na uchafu kila mahali na meza iliyojaa karatasi, magazeti, nk. Mtu aweze kutembea nyumba nzima bila kukanyaga midoli, nguo, nk.

Ni wajibu wa mwanamke kusaidia katika kuwalea watoto wafikie kuwa watumishi waaminifu wa Mungu. Mama, anapaswa kuwafundisha watoto wake kuwatii walio wazee, na watoto wanapaswa kuwaheshimu wale walio rika moja nao pia. Watoto wanapaswa kufundishwa kuwajibika katika matendo na mali zao.

## Maswali

1. Je, mwanamke, kwa idhini ya Mungu, anaweza kufanya kazi nje na nyumba yake?
2. Je, mwanamke, kwa idhini ya Mungu, anaweza asimtii mume wake?

# Majukumu ya Wanawake – Kazi za Kufanya

Tumeangalia vifungu mbalimbali katika Biblia vinavyofundisha wajibu wa wanawake na makatazo ambayo Mungu amewawekea. Sasa tuangalie kile ambacho Mungu anatarajia wanawake wakifanye.

## Mungu Anataka Wanawake Wote Waokolewe

***Marko 16:16***

"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."

***Wagalatia 3:27-29***

"Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi."

Sheria ya Ukristo haiweki tofauti kati ya mataifa, nyakati katika maisha au jinsia. Taifa moja si kuu kuliko taifa lingine. Mabwana si wakubwa kuliko watumwa. Wanawake si duni kwa wanaume. Wanadamu wote wako sawa kwa Kristo.

***2 Timotheo 4:1-5***

"Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa, kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake. Lihubiri neno, uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia,

> kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakatiwatakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti, nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. Bali, wewe uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa injili, timiza huduma yako."

Katika mazingira yote ya kifungu hiki, mtume Paulo anatoa maneno ya maelekezo na ya kutia moyo kwa mhubiri kijana Timotheo. Katika mstari wa 8, Paulo anawatia moyo Wakristo wote kubaki kuwa waaminifu ili wapate thawabu ya mbinguni, Yohana anafundisha kuwa mtu lazima abaki kuwa mwaminifu hata kufa (Ufunuo 2:10).

## Mungu Anatarajia Wanawake Waishi Maisha ya Utauwa

Tunatakiwa kufuata mifano ya wanawake hawa kwa namna walivyoishi maisha ya utauwa.

**Wanawake watauwa wanahitaji imani ya Sara**. Napiga picha hali hii akilini mwangu. Ibrahimu alirudi nyumbani siku moja akasema, "Sara, Mungu ameniambia tunatakiwa tuviache hivivyote, tusafiri nchi ya mbali." Sara aliuliza, "tunakwenda wapi?" Ambapo Ibrahimu alijibu, "sijui." "Tutafika lini huko?" aliuliza Sara. "Mungu hakuniambia." Ndivyoalivyojibu Ibrahimu. Bado, Sara kwa hiari aliiacha familia na marafiki na kusafiri wakiwa kama watu wanaoishi maisha ya kuhamahama bila kuwa na mahali ambapo Sara angepaita pakemwenyewe katika maisha yake yote. Hali hiyokama hiyo inahitaji

imani ya hali ya juu. Waebrania 11:11 inazungumzia imani kuu ya Sara alipopata mimba akiwa amevuka umri wa kupata mtoto.

**Wanawake watauwa wanahitaji kujitoa kama Ruthu**. Ruthu alijitoa kwa mama mkwe wake Naomi. Naomi na familia yake walihamia Moabu kwa sababu ya njaa katika nchi yao. Walipokuwa wakiishi huko watoto wawiliwa Naomi wa kiume walioa. Baadaye, mume wa Naomi na watoto wote wakafa. Naomi akaamua kurudi Bethlehemu kwa watu wake. Aliwashauri wakwe zake warudi kwenye nyumba za wazazi wao. Ruthu alikataa na akasafiri kwenda Bethlehemu pamoja na Naomi. Alisaidia kumtunza Naomi na alikuwa tayari amekubali ushauri kutoka kwake. Kristo alikuja kupitia uzao wa Ruthu (Mathayo 1:1-17).

**Wanawake watauwa wanahitaji ujasiriwa Esta**. Esta aliolewa na Ahasuero. Sheria ilipitishwa kuwa watu wake, Wayahudi, walitakiwa wauwawe. Esta akaenda mbele ya Mfalme kuwaombea ingawa hakuitwa. Kama mtu hakuitwa na Mfalme lakini akamwendea, Mfalme alimtaka mtu huyo auawe. Esta aliuona wokovu wa Wayahudi kuwa ni wa muhimu sana kuliko kulinda uhai wake.

**Wanawake watauwa wanahitaji matendo mema ya Dorkas**. Dorkas aliliona hitaji. Alikuwa na uwezo wa kutimiza hayo mahitaji na kufanya kazi pale pale. Alipokufa, wajane walimlilia wakimpitisha na kumwonyesha Petro nguo alizozishona (Matendo 10:39)

**Wanawake watauwa wanahitaji kuwa na shauku ya kujifanza ambayo Mariamu alikuwa nayo**. Alichagua sehemu bora (Luka 10:35-42). Kwa hiari yake alimsikiliza Kristo wakati ambapo angefanya kazi nzuri ya kusaidia kuandaa chakula kwa ajili ya wageni wake kama dada yake Martha alivyofanya. Mara nyingi tunashindwa katika hili. Tunajali zaidi mambo ya ‘hapa’naya ‘sasa’ kuliko kujali umilele.

**Wanawake watauwa wanahitaji huruma na ukarimu wa Lidia**. Lidia alikuwa akimwamini Mungu. Paulo alimkuta mtoni akimwabudu Mungu kwa namnaya pekee aliyokuwa anaijua. Paulo alimwelekeza yeye pamoja na watu aliokuwa nao kuhusu Kristo na wokovu. Pale pale Lidia aliyakubali mafundisho hayona kuitii Injili. Hata hivyo, hakuishia pale. Aliifanyia kazi imani mpya aliyoipata kwa kuwasisitiza Paulo na wenzake wakae naye alipokuwa Filipi (Matendo 16:14-16)**.**

**Wanawake watauwa wanahitaji kuwa na utayari wa kuieneza imani ya Eunike na Loisi**. Kama wanawake watauwa tunahitaji uharaka wa kufundisha kama Eunike na Loisi walivyomfundisha Timotheo (2 Timotheo 1:5). Hapa tunawaona mama na bibi ambao waliona hitaji kubwa la kufundisha (si kwa maneno tu, bali kwa mfano pia). Hatimaye Timotheo akawa mkubwa na kuwa mtumishi mahili wa Mungu na msaidizi wa mtume Paulo. Neno la Kiyunani kwa'mtoto' katika 2 Timotheo 3:15 linaweza kumaanisha kutoka 'uchanga' hadi kufikia hatua ya kuwa 'kijanamdogo'. Wanawake hawa watauwa waliona umuhimu wa kumfundisha Timotheo akiwa na umri mdogo. Tunatakiwa kuwa na uharaka huu wa kufundisha si watoto au wajukuu wetu tu, bali watoto wote. Hili linaweza kutekelezeka kwa kujifunza nyumbani au katika madarasa ya Biblia.

**Wanawake watauwa wanapaswa kuwa wasaidizi kama Prisila**. Je, ulijua kuwa hakuna aliyemtaja Prisila bila Akila au Akila bila Prisila katika Biblia? Prisila na Akila walifanya kazi pamoja (wakitengeneza hema), waliabudu pamoja na walimtumikia Mungu pamoja (Warumi 16:3-4). Prisila alimsaidia mume wake Akila kumfundisha Apolo njia ya Bwana kwa usahihi zaidi (Matendo 18:24-28).

**Wanawake watauwa wanapaswa kujitahidi kuwa mwanamke wa Mithali 31**. Katika sura hii, mama (inawezekana Bathsheba) alimwelekeza kijana wake wa kiume (inawezekana Sulemani akitumia

jina Lemueli Mithali 31:1, 1 Wafalme 2:13) katika sifa za kutafuta mke – kama tu alimsikiliza mama yake!

Kijana huyu alitakiwa kumtafuta mwanamke ambaye alikuwa na sifa za:

**Mke**. "***Moyo wa mume wake humwamini, wala hatakosa kupata mapato. Humtendea mema wala si mabaya, siku zote za maisha yake. Mume wake hujulikana malangoni, aketipo pamoja na wazee wa nchi***" (Mithali 31:11-12, 23). Anajua kuwa mke ataitunza nyumba yake kwa usahihi ili yale yaliyo ya muhimu katika maisha yawe yanapatikana. Wale wanaomwona wanajua kuwa ana mke mwema ambaye anamjali – nguo zake ni safi zilizoshonwa vizuri.

**Mama**. "***Wanawe huondoka na kumwita heri***" (Mithali 31:28). "***Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, uzao wa tumbo ni thawabu. Kama mishale mkononi mwa shujaa, ndivyo walivyo wana wa ujanani. Heri mtu yule aliyelijaza podo lake hivyo. Naam, hawataona aibu wanaposema na adui langoni***" (Zaburi 127:3-5). Watoto ni Baraka kutoka kwa Mungu, ambaye anatutaka tuwalee katika njia za Bwana. Mama mkamilifu huwafundisha wanawe kwa maneno, lakini muhimu zaidi ni kwa yeye kuwa mfano. Watoto wanajifunza kupenda na kutii baba zao (na wengine) kwa kumwona mama yao anapoonyesha upendo na utii kwa baba yao.

**Mfanyakazi**. ***"Tena huamka kabla haujaisha usiku, huwapa watu wa nyumbani mwake chakula, na wajakazi wake sehemu zao. Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake, wala hali chakula cha uvivu***" (Mithali 31:15, 27). Katika masaa ya asubuhi mwanamke huyu hutafuta chakula na mavazi kwa ajili ya familia yake pamoja na wafanyakazi wake. Kwa furaha mwanamke huyu hupanga siku yake kabla watu wa nyumbani mwake hawajaamka. Humaliza kazi zake zilizoko mbele yake.

**Mfanya biashara.**“***Afanana na merikebu za biashara, huleta chakula chake kutoka mbali. Huangalia shamba, akalinunua, kwa mapato ya mikono yake hupanda mizabibu. Hufanya nguo za kitani na kuziuza; huwapa wafanya biashara mishipi***” (Mithalii 31:14, 16, 24). Mwanamke bora huweka vipaumbele vya majukumu yake ktika mpangilio. Mawazo yake ya kwanza ni ya kumjali mume wake, na ya pili ni kwa watoto wake na mahitaji yao. Hata hivyo, bado ana muda wa kufanya biashara zake. Hununua shamba na kupanda bustani, halafu huuza alichokivuna. Biashara nyingine ni kununua vitambaa, na kushona nguo na kuziuza madukani. Katika kazi zake zote bado anakumbuka kumtumikia Mungu kwa kuwajali maskini (Mithali 31:20).

**Mwanamke mwenye afya.*“Hujifunga nguvu viunoni kama mshipi; hutia mikono yake nguvu.*”** (Mithali 31:17). Mwanamke bora huujali mwili wake. Hufanya mazoezi, hula chakula kamili na kupumzika vya kutosha. Huelewa kuwa ikiwa atashindwa kujali mwili wake hataweza kujali familia yake.

**Mwanamke anayevutia.**“***Hujifanyia mazulia ya urembo; mavazi yake ni kitani safi na urujuani***” (Mithali 31:22). Mwanamke bora hujipatia mavazi sahihi. Tayari ameshawapatia mume na watoto wake mavazi sahihi, na sasa anavaa mwenyewe. 1 Timotheo 2:9 inawaelekeza wanawake “wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri.” “Neno “kupamba” maana yake “kuweka katika mpangilio kwa lengo la kupendezesha.” Tunatakiwa tuvae nguo ambazo zinapamba miili yetu ipendeze, huku tukiwa katika hali ya kujisitiri. Sketi fupi, kaputula fupi vinguo vya juu vifupi, nguo za kubana na nguo zinazoangaza, hayo si mavazi ya kusitiri.

**Mwanamke mwenye kujali.**“***Hufumbua kinywa chake kwa hekima, na sheria ya wema i katika ulimi wake***.” (Mithali 31:26). Mwanamke bora hufikiri kabla ya kusema chochote ambacho ni chema

na kujali hisia za wengine. Maneno anayoyatumia ni ya uaminifu, ya kweli hasengenyi kamwe wala kuchukia bila kujali wengine wanamtendeaje. Hufuata sheria ya "dhahabu" ya Mathayo 7:12.

**Mwanamke mcha Mungu.** "***Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili; bali mwanamke amchaye Bwana, ndiye atakayesifiwa***" (Mithali 31:30). Mwanamke bora humtanguliza Mungu kwanza katika maisha yake. Humheshimu na kujitahidi kumtumikia katika maisha yake yote. Anajua kuwa mambo ya dunia yanapita lakini makao ya mbinguni hudumu hata milele. Njia pekee ya kufika huko nyumbani ni kuishi maisha kwa kumtumikia Mungu kwa uaminifu (Ufunuo 2:10).

**Mwanamke mtoa dhabihu.** Mwanamke bora hutoa mahitaji ya familia yake, marafiki zake, majirani zake na wale wenye mahitaji kuzidi matakwa na shauku yake. Hufanya kwa furaha, mara zote akiwafikiria wengine kabla ya kujifikiria yeye.

Tunaona kuwa "mwanamke bora" wa Mithali 31 ni mwanamke aliyezidi kwa ubora. Sasa, kabla hujamtangaza kuwa alikuwa mwanamke bora na kwamba hujawahi kukamilisha yale yote aliyoyafanya, kumbuka kuwa amewekwa kama mwanamke mkamilifu. Tunajua kuwa hatuwezi kuufikia ukamilifu, lakini kila siku tunapaswa kujitahidi kuboresha maisha kulingana na mapenzi ya Mungu. Huo niujumbe kwetu leo – hiki ndicho ambacho kila mwanamke anapaswa kukifanyia kazi.

Lois McCord anamlinganisha "mwanamke mwema" wa Mithali 31 na mtu wa talanta tano katika Mathayo 25:14-28:

> Ni mwanamke mwenye talanta tano. Mungu hafanyi wanawake wengi wenye talanta tano,kama anavyofanya wengine talanta mbili na talanta moja. Lakini jambo la muhimu kukumbuka ni kwamba kila mmoja wetu ana talanta moja au zaidi na tunapaswa kuzizalisha talanta

ambazo Mungu ametupa. Tutakuja kutoa hesabu zake siku ya hukumu "Mathayo 25:19). Zitafute talanta zako na uzizalishe, ukitambua kuwa Mungu amekubariki na uwezo wa kufanya baadhi ya mambo ambayo wengine hawawezi kufanya, huku wengine wakifanya yale ambayo huyawezi.

## Mungu Anawaamuru Watumishi Wake Kufanya Kazi katika Ufalme

“Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako, kwa kuwa hakuna kazi, wala ushauri, wala maarifa wala hekima, huko kuzimu uendako wewe” (Mhubiri 9:10).

“Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi” (Yohana 9:4-5).

“Halafu akawaambia wanafunzi wake, “Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake” (Mathayo 9:37-38).

“Hamsemi ninyi, “bado miezi minne, ndipo yaja mavuno”? Tazama, mimi nawaambieni, inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno” (Yohana 4:35).

Kuna kazi nyingi nzuri wanawake Wakristo wanaweza kufanya. Mipaka pekee ni (1) Wanawake wawe watiifu kwa wanaume nyumbani na kanisani. (2) Hawawezi kujiweka kwenye nafasi ya kuwatawala

wanaume nyumbani na kanisani. Kila kazi kwa ajili ya Bwana ambayo inakubaliana na majukumu na wajibu ambao Mungu ameamuru kwa wanawake zinakubalika na kutiwa moyo kwa kuthibitishwa na wazee.

## Sasa basi, Mwanamke Mkristo Anaweza Kufanya Nini ili Amtumikie Mungu Wake?

Wanawake wanaweza kufundisha kwa namna nyingi. Tunafundisha kwa mifano, tunafundisha tunapoimba nyimbo za sifa (Wakolosai 3:16), tunaweza kufundisha madarasa ya Biblia ya watoto, tunaweza kufundisha darasa la Biblia la wanawake na tunaweza kufundisha madarasa binafsi [tukiwasaidia wanaume]. Maadamwanawake wanatambua mipaka ambayo Mungu amewawekea, chaguzi zetu ni nyingi na zimewekewa mipaka tu kulingana na uwezo wetu.

Kazi ya kwanza na ya muhimu kwa mwanamke Mkristo, ambaye ana familia ni kuwalea watoto wake katika Neno la Mungu. Tunaweza kufanya aina zote za kazi nzuri, lakini tukishindwa kuwafundisha watoto, tutakuwa tumeshindwa. Wale ambao ni mabibi wanapaswa kutambua umuhimu na ushawishi ambao wanaweza kuwa nao kuwafundisha wajukuu zao. Kumbuka Loisi alimfundisha Timotheo. Mara nyingi akina bibi ndio wanaowajibika kwa mafundisho ambayo wajukuu zao wanayapokea. Akina shangazi na mabinamu wanaweza kusaidia katika kazi ya kufundisha. Kwa uasherati uliotuzunguka, watoto wetu wanahitaji kila aina ya ushauri ambao tunaweza kuwapa. Vijana wanahitaji kuwa na nafasi ya kushirikiana na Wakristo wengine. Wawasaidie wazazi katika hali ya kuwakaribisha vijana wenzaowa kusanyiko kwa kufungua nyumba zenu kwa ajili ya furaha na ushirika wakati wa jioni.

Tunaweza kufundisha darasa la Biblia lawanawake. Cha kuzingatia ni kwamba, wanawake huwa wanajifunza kwa hisia zaidi katika masomo yao, wakati wanaume huwa wanapokea kwa kutafakari ujumbe kiakili zaidi [ndivyo tulivyoumbwa]. Kama walimu na wanafunzi, tunatakiwa kuzitia moyo pande zote mbili, yaani upande wahisia na upande wa akili katika somo. Madarasa ya wanawake peke yao yanaweza kujadili mada ambazo hazitamfaa sanamwanaume kufundisha. Pia kumbuka wanawake wazee wanatakiwa kuwafundisha wanawake vijana (Tito 2:4).

Mwalimu mzuri wa darasa la Biblia atamsaidia mwanafunzi kijana kukumbuka masomo ya msingi ya Biblia na kanuni baada ya kukua kwake. Kamwe usidharau kazi nzuri ya kufundisha watoto madarasa ya Biblia, iwe ni madarasa ya jioni ya siku za katikati za juma, Jumapili asubuhi au vipindi vyovyote vya Biblia wakati wa likizo. Wanawake wanaweza kuwasaidia walimu kuandaa baadhi ya mahitaji ya aina nyingi za vifaa vya kufundishia ambavyo mwalimu anahitaji kuvitumia, hasa kwa madarasa ya watoto. Inawezekana talanta yako ni kupanga na kutunza chumba chenye rasilimali za kufundishia za walimu. Walimu wengi wangependa kiwepo chumba ambacho ni rahisi kupata picha au karatasi za masomo.

Masomo ya Biblia ya nyumbani, ikiwa ni nyumbani kwako au kwa mtu mwingine, ni njia nzuri ya kuwafundisha wale ambao si Wakristo na kuwatia moyo wakristo wachanga. Kama unajiona huwezi kufundisha, mwombe mtu mwingine afundishe. Kwa wale wanaoona kuwa hawawezi kufundisha hadharani, kusahihisha na kutuma masomo ya Biblia pia ni uchaguzi mzuri. Kama swali litaulizwa, utakuwa na muda wa kujifunza na kuandaa jibu.

Vitabuvya kufundishia vinavyoeleweka kirahisi, tena vyenye kubeba mafundisho ya kweli ya Biblia ni vya muhimu sana na

vinahitajika leo. Nitawatia moyo,kwa yeyote ambaye ana uwezo kuandika na kuongeza talanta yake katika eneo hili. Wanawake wanaweza kuandika vijarida vya Biblia kwa ajili ya magazeti ya Injili. Kama unaona huna uwezo wa kuandika, unaweza kutoa huduma yako kama mtafiti, mchapishaji, au mhariri wa hao wanaoandika.

Mbao za matangazoni zana nzuri za kufundishia. Picha ikiwa na maandishi machache inaweza kusema zaidi kuliko kumweka mtu na kumfundisha papo kwa papo. Kwa teknolojia ya sasa, hata kwa wale ambao si wachoraji wanaweza kuandaa mbao nzuri za matangazo zinazoweza kuchokoza wazo. Kuwepona mashine ya rangi na karatasi nyingi zinazopatikana, unaweza kupata picha nzuri ya rangi kwa kila kitu. Kusanya mawazo kutoka katika makusanyiko mengine ambayo unayatembelea, majarida au magazeti ya kidini, vitabu kuhusu mbao za matangazo au elezea mstari wa Biblia.Kama unaona huwezi kuandaa ubao wa matangazo halisi, nenda na mawazo kwa rafiki mbunifu ili amalizie na akusaidie kukamilisha mpango wako.

Je, unapenda kuwa karibu na watu? Labda talanta yako ipo vizuri kwa kutembelea hospitali, kusaidia nyumbani au kuwasaidia wafungwa. Waongofu wapya, wanawake vijana na washiriki dhaifu wanaweza kutumia sura ya kirafiki na maneno ya faraja. Kama unaona kuwa hujui cha kusema, toa usafiri na umsindikize mtu mwingine afanye.

Kwa wale wenye ujuzi wa vitu vya umeme, toa huduma yako kama msaidizi wa kanisa. Chapisha vijarida, jibu masomo na tunza mafaili ya taarifa mhimu, nk.

Wanawake wanaweza kupanga na kutunza sehemu ya kuhifadhia chakula na nguo kwa wale wenye uhitaji. Pia wanaweza kusaidia kuvigawa vitu hivyo.

Wanawake wanaweza kutunza nyumba ya kukutania, kuliweka jingo la Kanisa katika hali ya usafi, na kupamba ndani na nje kwa maua na mapambo mengine. Tunaweza kujitoa kufua nguo za kubatiziana kuzirekebisha, kuwasaidia wanawake wanaobatizwa, na kuandaa meza ya Bwana pamoja na kuvisafisha vyombo vya meza ya Bwana.

Wajue washiriki wa kusanyiko lako. Hatuwajui kwa sawa sawa ndugu zetu waume na wake katika Kristo kwa kuwa tunawaona kwenye jingo la kanisani tu. Kujua jinsi watu walivyo kiuhakika, wakaribishe nyumbani kwako. Waandalie chakula, wape vitafunwa au kinywaji – kile unachoona kinaweza kuwafurahisha wewe na wageni wako. Chochote utakachoamua, wafanye wajisikie wamekaribishwa.

Waalike wahubiri, wamishenari na wafanyakazi wengine wa kanisa nyumbani kwako wakutembelee. Tena, chakula kingi si muhimu. Mahali pa kupumzika, ushirika mzuri na vinywaji baridi mara zote vinatosha.

Wasikilize wale wenye uhitaji. Hakikisha kuwa siri ambazo unaambiwa zinabaki na wewe. Usiseme kile ulichoambiwa kwa siri. Kama ukiona mtu mwingine anapaswa kujua shida hiyo, mshauri mhusika [anayekuambia] amwendee huyo mtu mwenyewe. Kumwambia mtu kuhusu tatizo itasaidia kuliweka katika mtazamo sahihi.

Watie moyo wazee, mashemasi, wahubiri na walimu katika kazi nzuri wanayoifanya. Angalia mambo madogo madogona utoe neno. Kama somo zuri limefundishwa, sema. Kama maamuzi magumu au yasiyo ya kawaida yametolewa, waambie unashukurukwamsimamo waliouchukua na kubaki katika uamuzi huo.

Msaidie mume wako aweze kufikia kuwa na sifa za kuwa mzee au shemasi. Najua hakuna kazi kubwa kwa Bwana kama kuongoza watu wa Mungu katika thawabu za mbinguni. Kumbuka kuwa mzee au

shemasi aliye na sifa, ni lazima awe na mke mwenye sifa (1 Timotheo 3:1-11).

Imani, ibada, ujasiri na shauku ya kujifunza neno la Mungu vitatusaidia kukua. Kwa kukua tutaanza kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Kuwa na huruma, kuwa wakarimu na kufundisha yatakuwa matokeo yanayoonekana kwa macho.

Kuna wimbo unaoitwa, “Tuma nuru.” Wengine, “Chukua Nuru” huku wengine “Tuma nuru.” Wewe ni yupi? Mchukuaji au mtumaji? Wote tuna majukumu binafsi ya kuwaongoza watu kwa Kristo.

**Kuna kazi nyingi kwa watu wote. Tafuta talanta zako, zikuzalishiena uzitumie kwa ajili ya Kristo. Kumbuka Mungu ametupa majukumu ya kufanya. Kwa hiari tekeleza wajibu huo na ukumbuke maelekezo ambayo Mungu ametupa**. Tukiwa tunafanya yote tunayoweza, hatutakuwa na muda wa kutaka kupinga maelekezo hayo. Kuna kazi nyingi zaidi ya tunazoweza kufanya, hivyo tujishughulishe na kazi ya Mungu!

## Maswali

1. Ni kazi gani inatakiwa kufanyika mahali unapoabudu ambayo mwanamke anaweza kufanya?
2. Je, tayari umeshapata nafasi yako katika huduma ya Bwana wetu?

# Mpango wa Mungu wa Wokovu

**Sikia Neno la Mungu**

- "Basi imani, chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo" (Warumi 10:17).

**Amini au uwe naimani**

- "Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini, atahukumiwa" (Marko 16:16).

**Tubu**

- "Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wa kila mahali watubu" (Matendo 17:30).

**Kiri imani yako kwa Kristo kama Bwana**

- "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu" (Warumi 10:9-10).

**Ubatizwe katika maji**

- "Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukiliitia jina lake" (Matendo 22:16).

**Ishi maisha ya uaminifu**

- "…Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima" (Ufunuo 2:10).